BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MASWALI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI MWAKA 2017

# KISWAHILI

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MASWALI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI MWAKA 2017

# KISWAHILI

*Kimechapishwa na*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2017**

Haki zote zimehifadhiwa.

# YALIYOMO

DIBAJI ..................................................................................................... iv

1.0 UTANGULIZI ..................................................................................................... 1

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA ..................................................... 1

2.1 Sehemu A: Sarufi ..................................................................................................... 2

2.2 Sehemu B: Lugha ya Kifasihi ..................................................................... 29

2.3 Sehemu C: Ufahamu ..................................................................... 42

2.4 Sehemu D: Ushairi ..................................................................... 57

2.5 Sehemu E: Utungaji ..................................................................... 65

3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA MADA MBALIMBALI ..................................................................... 67

4.0 HITIMISHO ..................................................................... 69

5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO ..................................................................... 70

KIAMBATISHO A ..................................................................... 72

KIAMBATISHO CHA PEKEE ..................................................................... 74

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa ya uchambuzi wa majibu ya maswali ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa somo la Kiswahili mwaka 2017. Lengo kuu la taarifa hii ni kutoa mrejesho kwa walimu, wanafunzi, watunga sera, wathibiti ubora wa elimu, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu jinsi watahiniwa walivyojibu maswali ya mtihani huo. Majibu ya watahiniwa ni ishara inayoonesha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kuhusu mambo ambayo watahiniwa waliweza kujifunza kwa ufanisi na yale waliyoshindwa kuyapata katika kipindi cha miaka saba ya elimu ya msingi.

Taarifa hii, imechambua sababu mbalimbali zilizochangia watahiniwa kujibu kwa usahihi au kushindwa kujibu maswali hayo kama ilivyotakiwa. Matokeo ya uchambuzi yamebainisha baadhi ya sababu zilizochangia watahiniwa kutojibu maswali kwa usahihi, kama vile kushindwa kutambua matakwa ya swali, kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada mbalimbali katika somo, kukosa maarifa kuhusu kanuni za lugha na matumizi ya misamiati, kutojibu kabisa baadhi ya maswali au kuchagua jibu zaidi ya moja kinyume na maelekezo na kushindwa kutambua vitu katika mazingira wanamoishi ambavyo ni vyanzo vya majibu ya maswali mengi. Uchambuzi uliofanyika kwa kila swali umebaini pia mambo yaliyosaidia watahiniwa kujibu maswali kwa usahihi kama vile kutambua matakwa ya swali, kuwa na uelewa wa mada mbalimbali katika somo, kuzingatia kanuni za lugha na matumizi sahihi ya misamiati katika lugha ya Kiswahili. Aidha, taarifa ya uchambuzi imebainisha idadi na asilimia ya watahiniwa ambao hawakuzingatia maelekezo ya maswali. Maelekezo hayo hujumuisha kuandika machaguo zaidi ya moja katika swali husika na walioacha kujibu maswali mbalimbali.

Uchambuzi huo umefafanuliwa katika maelezo, jedwali au kielelezo kilichoambatanishwa katika kipengele cha majibu ya kila swali.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatarajia kuwa, mrejesho uliotolewa utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kutafuta mbinu za kuboresha ufundishaji na ujifunzaji ili kupata ufumbuzi wa kasoro mbalimbali zilizobainishwa katika taarifa hii. Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa maoni yaliyotolewa yakifanyiwa kazi ipasavyo, wanafunzi wanaohitimu elimu ya msingi watapata ujuzi na maarifa yanayotakiwa na hivyo kuinua kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani za dhati kwa wote walioshiriki kuandaa taarifa hii wakiwemo Maafisa Mitihani, Wataalam wa TEHAMA na Wataalam Maalum wa Elimu walioshiriki katika uchambuzi. Baraza linatarajia kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa wadau mbalimbali wa elimu ili kuboresha taarifa ya uchambuzi wa maswali ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa somo la Kiswahili.

Dkt. Charles E. Msonde

**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii imeandaliwa ili kutoa mrejesho kuhusu watahiniwa walivyojibu maswali katika mtihani wa somo la Kiswahili. Mtihani wa Kiswahili ulikuwa na maswali **hamsini** (**50)** ya kuchagua jibu sahihi ambayo yalikuwa yamegawanywa katika sehemu tano ambazo ni: Sehemu A: Sarufi; B: Lugha ya Kifasihi; C: Ufahamu; D: Ushairi na E: Utungaji. Jumla ya watahiniwa **916,885** walisajiliwa kufanya mtihani wa **PSLE 2017** somo la Kiswahili na waliofanya mtihani walikuwa **909,909**. Watahiniwa waliofaulu mtihani huu ni **790,292** sawa na asilimia **86.86**.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA

Sehemu hii imeainisha maswali yote ya mtihani na majibu ya kuchagua kwa kila swali yaliyotolewa kwa watahiniwa. Idadi na asilimia ya watahiniwa waliochagua kila chaguo (jibu) na waliochagua jibu zaidi ya moja au kuandika mambo mengine imeoneshwa bayana. Aidha, uchambuzi wa sababu zilizochangia watahiniwa kuchagua majibu sahihi na yasiyo sahihi umeainishwa. Asilimia ya kufaulu kwa watahiniwa katika kila swali imewasilishwa kwa kutumia maelezo, jedwali au kielelezo (grafu). Rangi mbalimbali zimetumika kuonesha hali halisi ya asilimia ya watahiniwa walioweza kujibu kila swali ambapo asilimia kati ya **0 – 39** ya idadi ya watahiniwa waliochagua chaguo sahihi imewasilishwa kwa rangi nyekundu (hafifu), asilimia **40 – 59** rangi ya njano (wastani) na asilimia **60 – 100** rangi ya kijani (Nzuri). Alama * imetumika katika jedwali kuonesha jibu sahihi lililotakiwa kwa kila swali.


## 2.1 Sehemu A: Sarufi

**Swali la 1:** Neno lipi ni **tofauti** na maneno mengine kati ya haya?

A. Chungwa
B. Embe
C. Ndizi
D. Nanasi
E. Mgomba

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu matumizi ya msamiati wa Kiswahili. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 829,382 sawa na asilimia 90.44 waliweza kuchagua jibu sahihi *E, Mgomba*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu matunda mbalimbali na mimea inayozaa matunda hayo hususan mgomba ambao ni mmea unaozaa ndizi, hivyo ‘mgomba’ haufungamani na aina nyingine za matunda zilizoorodheshwa.

Watahiniwa wachache, 79,026 (8.62%) pekee ndio waliochagua vipotoshi kati ya *A Chungwa*, *B Embe, C Ndizi* na *D Nanasi*. Uteuzi wa vipotoshi hivyo unaonesha watahiniwa walishindwa kutofautisha mmea unaozaa matunda na matunda yaliyo tayari kwa ajili ya matumizi. Aidha, uteuzi wa vipotoshi hivyo ulitokana na kuwa matunda hayo kwa pamoja (chungwa, embe, ndizi na nanasi) huondolewa maganda yake ndipo yaliwe japokuwa si sawa na mgomba ambao huzaa ndizi. Mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo umeoneshwa katika **Kielelezo 2.1**.





**Kielelezo 2.1** *kinaonesha kiwango kizuri cha kufaulu katika swali hili ambapo asilimia 90.44 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi E, Mgomba.*

**Swali la 2**: Mto Ruvu umefurika mwaka huu. Katika sentensi hii, maneno "mwaka huu" ni ya aina gani?

A. Nomino
B. Vitenzi
C. Vivumishi
D. Vielezi
E. Viwakilishi

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua aina za maneno kama yalivyotumika katika sentensi. Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani ambapo watahiniwa 482,234 sawa na asilimia 52.58 waliweza kuchagua jibu sahihi *D, Vielezi* kutokana na uelewa wa kutambua dhana ya vielezi kuwa ni maneno yanayoelezea tendo lililofanyika (kitenzi) ambapo neno 'mwaka huu' linaeleza wakati ambapo mto Ruvu umefurika. Aidha, katika mpangilio wa maneno katika sentensi, *kielezi* hutokea baada ya kitenzi. Uchaguzi wa jibu sahihi unaonesha kuwa, watahiniwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu aina za maneno.

Hata hivyo, watahiniwa 424,013 sawa na asilimia 46.24 walichagua vipotoshi *A Nomino, B Vitenzi, C Vivumishi* na *E Viwakilishi*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *A*, *Nomino* walishindwa kutambua kwamba kielezi kinaweza kujengwa kwa maneno mawili 'mwaka huu' badala yake wakaridhika na neno 'mwaka' ambalo hutumika kama nomino linapokuwa peke yake. Uteuzi wa kipotoshi *B, Vitenzi* ulitokana na mfuatano wa kitenzi 'kufurika' na neno 'mwaka huu (kielezi) kuonekana kama ni mwendelezo wa kitenzi cha awali. Aidha, uteuzi wa vipotoshi *C, Vivumishi na E, Viwakilishi* unadhihirisha wazi kuwa watahiniwa hao hawakuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu aina za maneno hasa pale maneno mawili yanapotumika kwa pamoja kama aina moja ya neno. Mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo umeoneshwa katika **Kielelezo 2.2**.




**Kielelezo 2.2** *kinaonesha kiwango cha wastani cha kufaulu ambapo asilimia 52.58 ya watahiniwa waliweza kubaini kwa usahihi maneno "mwaka huu" kuwa ni vielezi.*

**Swali la 3**: “Mimi sitakuja.” Sentensi hii iko katika kauli gani?

A. Kanushi
B. Ombi
C. Swali
D. Taarifa
E. Halisi

**Jedwali 2.1: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 237,547 | 33,228 | 23,347 | 278,247 | 334,067 | 10,650 |
| Asilimia ya watahiniwa | 25.90 | 3.62 | 2.55 | 30.34 | 36.43 | 1.16 |

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kubainisha kauli mbalimbali katika sentensi. Kiwango hafifu cha kufaulu kwa watahiniwa kimefafanuliwa katika **Jedwali 2.1** ambapo watahiniwa wachache (36.43%) waliweza kubaini kwa usahihi kauli ya sentensi, “Mimi sitakuja” kuwa ni *E, Halisi.*

Watahiniwa 572,369 sawa na asilimia 62.41 walichagua kati ya viposhi *A Kanushi, B Ombi, C Swali na D Taarifa* kwa kuwa walishindwa kubaini kauli ya sentensi “Mimi sitakuja” kuwa ni kauli halisi badala yake wakatoa majibu yasiyokidhi matakwa ya swali. Uteuzi wa kipotoshi *A, Kanushi* ulihusisha umbo la **si-** ambalo hutumika katika tungo za Kiswahili kuonesha dhana ya ukanushi. Uteuzi wa kipotoshi *B, Ombi* unadhihirisha kwamba watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya neno ‘ombi’ lenye maana ya maneno au ishara anayotoa mtu kwa mtu mwingine mwenye uwezo ili amsaidie halihusiani na kauli yoyote ya sentensi bali ni aina za sentensi. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *C, Swali* ambacho kina maana ya hoja ya jambo au kitu kinachoulizwa na kuhitaji jibu hakikuakisi kauli ya sentensi husika. Aidha, watahiniwa waliochagua kipotoshi *D*, *Taarifa*

walishindwa kubaini kuwa umbo la kauli taarifa katika lugha ya Kiswahili, lazima liambatane na maneno ‘kuwa’ au ‘kwamba’ ili kutoa maana iliyokusudiwa.

Asilimia 36.4 ya watahiniwa walioweza kuchagua jibu sahihi *E*, *Halisi* waliweza kubaini kauli halisi katika sentensi hiyo kutokana na ukweli kuwa ni maneno yanayotamkwa na mzungumzaji moja kwa moja na kueleweka bila ufafanuzi mwingine wowote.


**Swali la 4**: “Mama mdogo amepika ugali mwingi.” Maneno gani ni vivumishi katika sentensi hii?

A. Mdogo na mwingi
B. Mama na mdogo
C. Ugali na mwingi
D. Mdogo na amepika
E. Amepika na ugali

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuainisha vivumishi katika sentensi waliyopewa. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kwa jumla kilikuwa ni cha wastani. Katika kujibu swali hili, idadi kubwa ya watahiniwa, 464,962 sawa na asilimia 50.70 walichagua vipotoshi *B mama na mdogo, C ugali na mwingi; D mdogo na amepika na E amepika na ugali*. Uteuzi wa vipotoshi *B mama na mdogo* na *C ugali na mwingi* unaonesha kuwa watahiniwa hawana maarifa ya kutosha kuhusu aina za maneno hususan nomino na vivumishi. Watahiniwa hao walishindwa kutofautisha nomino na kivumishi ambapo nomino ni neno linalotaja jina la mahali, mtu, kitu au tendo na kivumishi ni neno linalotoa taarifa zaidi kuhusu nomino. Watahiniwa waliochagua vipotoshi *D mdogo na amepika* na *E amepika na ugali*, hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu matumizi ya nomino, vivumishi na vitenzi katika sentensi na hivyo kushindwa kubaini vivumishi katika sentensi

hiyo. Aidha, walikosa maarifa kuhusu maana ya kitenzi kuwa ni neno linaloeleza tendo ama lililofanyika au litakalofanyika hivyo, hakuna uhusiano wa karibu kati ya vivumishi na vitenzi.

Hata hivyo, kiasi cha watahiniwa 440,299 sawa na asilimia 48.01 walichagua herufi ya jibu sahihi *A mdogo na mwingi*. Watahiniwa hao waliweza kuainisha vivumishi kwa kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu aina za vivumishi na za maneno kwa jumla. Aidha, katika mpangilio, maneno yote mawili yalitanguliwa na nomino na hivyo kuweza kubaini jibu sahihi kwani vivumishi 'mdogo' na 'mwingi' vimefanya kazi ya kuelezea nomino 'mama' na 'ugali' kama maneno hayo yalivyotumika katika sentensi hiyo. **Kielelezo 2.3** kinaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.




***Kielelezo 2.3** kinaonesha kiwango cha wastani cha kufaulu ambapo asilimia 48.01 ya watahiniwa waliweza kubaini vivumishi katika sentensi "*Mama mdogo amepika ugali mwingi"*.*


**Swali la 5**: "Wakulima wamehamisha mizinga ya nyuki kutoka mashambani mwao". Umoja wa sentensi hii ni upi?

A. Mkulima amehamisha mizinga ya nyuki kutoka shambani mwao.
B. Mkulima amehamisha mzinga wa nyuki kutoka shambani mwake.
C. Mkulima amehamisha mizinga ya nyuki kutoka shambani mwake.
D. Mkulima amehamisha mzinga wa nyuki kutoka shambani mwao.
E. Mkulima amehamisha mzinga ya nyuki kutoka shambani mwake.

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kutambua sentensi katika umbo la umoja na wingi. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa ni kizuri ambapo kiasi cha watahiniwa 672,951 sawa na asilimia 73.38 waliweza kuchagua jibu sahihi *B Mkulima amehamisha mzinga wa nyuki kutoka shambani mwake*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya upatanisho wa kisarufi katika tungo za lugha ya Kiswahili. Hivyo, watahiniwa walizingatia maneno yenye umoja na wingi katika makundi ya ngeli husika. Kwa mfano, umbo la **m-** (Umoja) huwa **mi-** (wingi), pia umbo la **m-** (umoja) huwa **wa-** (wingi). Hivyo, maneno 'mkulima' na 'mzinga'(nomino) yana maumbo ya umoja na wingi. Aidha, wingi wa maneno mengine katika sentensi hiyo, hudhihirika katika viambishi vya nafsi.

Hata hivyo, watahiniwa 233,627 sawa na asilimia 25.47 walichagua vipotoshi *A Mkulima amehamisha mizinga ya nyuki kutoka shambani mwao*, *C Mkulima amehamisha mizinga ya nyuki kutoka shambani mwake*, *D Mkulima amehamisha mzinga wa nyuki kutoka shambani mwao* na *E Mkulima amehamisha mzinga ya nyuki kutoka shambani mwake*. Watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na maarifa

ya kutosha kuhusu dhana ya upatanisho wa kisarufi au viambishi vya maumbo ya umoja na wingi katika maneno ya Kiswahili. Mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo umefafanuliwa vizuri katika **Kielelezo 2.4**.




**Kielelezo 2.4** *kinadhihirisha kiwango kizuri cha kufaulu cha watahiniwa ambapo idadi kubwa ya watahiniwa waliweza kubaini kwa usahihi umoja wa sentensi* 'Wakulima wamehamisha mizinga ya nyuki kutoka mashambani mwao.'


**Swali la 6**: "Mwajuma amemwibia Mwanahamisi kalamu yake". Katika sentensi hii, 'Mwajuma ni nani?

A. Mtendewa
B. Mtendana
C. Mtendeka
D. Mtenda
E. Mtendwa

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kubainisha kauli za utendekaji katika lugha ya Kiswahili. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa usahihi na watahiniwa wengi ambapo watahiniwa 714,319 sawa na asilimia 77.89 waliweza kuchagua jibu sahihi *D Mtenda*. Uteuzi wa jibu hili unaonesha kuwa watahiniwa

walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maumbo ya vitenzi yenye kauli za utendekaji, hivyo kuweza kubaini mtenda katika sentensi hiyo ambaye ni *Mwajuma.*

Watahiniwa wachache, asilimia 21 walichagua vipotoshi *A Mtendwa; B Mtendana; C Mtendeka na E Mtendwa*. Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha katika kubaini kauli za utendaji. Uteuzi wa kipotoshi *A, Mtendewa* ambacho huonesha kauli ya utendekaji kwa umbo –ew kinadhihirisha kuwa mtu fulani amefanyiwa jambo na mtu mwingine. Katika sentensi "Mwajuma amemwibia Mwanahamisi kalamu yake", *Mwanahamisi* ni mtendewa na *Mwajuma* ndiye mtenda. Hivyo watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu wahusika wa utendekaji wa jambo ili kubaini kauli ya kutenda katika sentensi. **Kielelezo 2.5** kinaonesha jinsi watahiniwa wengi walivyoweza kujibu swali hili kwa usahihi.




**Kielelezo 2.5** *kinaonesha kiwango kizuri cha kufaulu cha asilimia 77.89 ambapo watahiniwa wengi waliweza kumbaini Mwajuma kama mtenda katika sentensi hiyo.*

**Swali la 7**: Kinyume cha neno “duwaa” ni kipi?

A. Shangaa
B. Staajabu
C. Bashasha
D. Pumbaa
E. Butwaa

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika utambuzi wa kinyume cha maneno katika msamiati wa lugha ya Kiswahili. Swali hili ni miongoni mwa maswali yenye kiwango hafifu cha kufaulu. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa watahiniwa 626,786 sawa na asilimia 68.35 ya watahiniwa wote waliojibu swali hili walichagua vipotoshi *A Shangaa, B Staajabu, D Pumbaa na E Butwaa*. Watahiniwa 344,206 (37.53%) walichagua *A, shangaa* chenye maana ya kushikwa na butwaa kutokana na kusikia au kuona kitu cha ajabu ambacho hakitegemewi. Watahiniwa hao walishabihisha neno ‘shangaa’ lenye maana sawa na ‘duwaa’ bila kubaini kinyume cha maneno hayo. Watahiniwa 133,303 (14.54%) walichagua *B, Staajabu*, kikiwa na maana ya kushangaa kutokana na jambo, kusikia au kuhisi kitu bila kutambua kuwa neno hilo lina maana sawa na ‘duwaa’ na sio kinyume chake kama ilivyotakiwa. Watahiniwa wengine 101,155 (11.03%) walichagua *E, Butwaa*, chenye maana ya mshangao unaompata mtu na akabaki ameduwaa au kupatwa na bumbuwazi. Mwisho, watahiniwa wachache 48,122 sawa na asilimia 5.25 walichagua *D, Pumbaa* kikiwa na maana ya duwaa, shangaa au staajabu. Hivyo, uteuzi wa vipotoshi hivyo unadhihirisha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa dhana ya kinyume cha neno “duwaa” kwa kuwa walishabihisha vipotoshi vyote na neno hilo badala ya kubainisha kinyume cha neno hilo.

Hata hivyo, watahiniwa wachache (277,793) sawa na asilimia 30.29 pekee ndio walioweza kuchagua jibu sahihi *C Bashasha*, lenye maana ya hali ya kuonesha furaha, ucheshi na uchangamfu ambalo ni kinyume cha neno "duwaa". Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya kinyume, maana na matumizi ya msamiati katika lugha ya Kiswahili.

**Swali la 8**: "Uvumilivu ulimfanya Pendo apate zawadi." Uvumilivu ni aina gani ya neno?

A. Nomino
B. Kitenzi
C. Kivumishi
D. Kihisishi
E. Kiwakilishi

**Jedwali 2.2: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 216,096 | 170,608 | 324,923 | 52,532 | 140,036 | 12,891 |
| Asilimia ya watahiniwa | 23.56 | 18.60 | 35.43 | 5.73 | 15.27 | 1.41 |

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua aina za maneno kama yalivyotumika katika sentensi. Muhtasari wa majibu ya watahiniwa umeoneshwa katika **Jedwali 2.2.** Watahiniwa wengi, 324,923 sawa na asilimia 35.43 walichagua kipotoshi *C kivumishi,* kwa kuwa walishabihisha 'kivumishi' na 'uvumilivu' kutokana na maumbo ya maneno hayo. Hata hivyo, uteuzi wa *B Kitenzi*, *D Kihisishi* na *E Kiwakilishi* kunadhihirisha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kuainisha maneno katika sentensi husika.

Watahiniwa wachache 216,096 sawa na asilimia 23.56 ndio walioweza kuchagua jibu sahihi *A, Nomino*. Watahiniwa hao walikuwa

na maarifa ya kutosha kuhusu aina za maneno na aina za nomino yaani nomino dhahania (uvumilivu).


**Swali la 9**: “Yupi kati ya wafuatao ni lazima awe mwanaume?

A Mjomba
B Binamu
C Mjukuu
D Ndugu
E Mzee

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu maana na matumizi ya msamiati. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri, kwani watahiniwa 718,776 (78.38%) waliweza kuchagua jibu sahihi *A, Mjomba*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu uhusiano wa ndugu katika familia kwa upande wa mama.

Watahiniwa waliobaki 187,208 sawa na asilimia 20.41 walichagua vipotoshi *B Binamu*, *C Mjukuu*, *D Ndugu* na *E Mzee*. Watahiniwa hao walishindwa kutambua uhusiano wa ndugu katika familia kwa upande wa mama. Hivyo basi, watahiniwa waliochagua *B, Binamu* walishindwa kutambua kuwa binamu ni mtoto wa kike au wa kiume wa shangazi au mjomba kwa upande wa baba na mama. Aidha, watahiniwa waliochagua *C, Mjukuu* walishindwa kutambua kuwa mjukuu ni mtoto wa kike au wa kiume wa mtoto wako. Watahiniwa wachache walichagua *D, Ndugu* kutokana na kutotafakari maana pana iliyoko katika neno ‘ndugu’ ambapo kwanza ni mtu uliyezaliwa naye kwa baba au mama au na wazazi wote wawili. Pili, mtu uliyezaliwa naye ndani ya ukoo wako. Tatu, ni mtu uliye na uhusiano naye wa karibu. Mwisho, neno ndugu lina maana ya mwenza na mshirika wa karibu katika masuala ya kijamii. Watahiniwa wengine waliochagua *E, Mzee* hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu neno

hilo ambalo hutumika kwa mwanamume au mwanamke aliyezeeka. Kufaulu kwa watahiniwa na mtawanyiko wa majibu kwa kila chaguo kumeoneshwa katika **Kielelezo 2.6.**




**Kielelezo 2.6** *kinaonesha kiwango kizuri cha kufaulu cha asilimia 78.38 cha watahiniwa walioweza kubaini uhusiano wa watu katika familia ambapo* 'mjomba' *lazima awe mwanaume.*


**Swali la 10**: "Walimu watafundisha masomo yao vizuri." Sentensi hii ipo katika wakati gani?

A. Uliopita
B. Ujao
C. Uliopo
D. Mazoea
E. Timilifu

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika utambuzi wa maumbo ya kitenzi yanayoonesha njeo wakati tendo linapofanyika. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 735,025 (80.15%) waliweza kuchagua jibu sahihi *B Ujao*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maumbo ya

kitenzi yanayoonesha njeo, na hivyo kubaini kuwa umbo **-ta-** katika kitenzi watafundisha linaonesha njeo ya wakati ujao.

Aidha, watahiniwa 107,108 sawa na asilimia 18.76 walichagua vipotoshi *A Uliopita, C Uliopo, D Mazoea na E Timilifu*. Watahiniwa hao walishindwa kubaini kuwa wakati uliopita katika hali timilifu huoneshwa na umbo –**me-**, wakati uliopita umbo –**li-** na wakati uliopo huoneshwa na umbo –**na-**, maumbo ambayo hayakuwepo katika kitenzi husika. Aidha, watahiniwa waliochagua *D, Mazoea na E, Timilifu* walishindwa kutambua kuwa mazoea siyo njeo bali ni hali ya kitenzi inayooneshwa kwa umbo la **hu-** katika kitenzi. Umbo hilo halikuwepo kwenye kitenzi husika. Kiwango cha kufaulu katika swali hili kimeoneshwa katika **Kielelezo 2.7**




**Kielelezo 2.7** *kinaonesha kiwango kizuri cha kufaulu ambapo watahiniwa wengi asilimia 80.15 waliweza kubaini njeo ya wakati ujao katika sentensi.*

**Swali la 11**: "Wanafunzi wenzake walimnyanyapaa." Neno walimnyanyapaa lina maana ipi kati ya hizi zifuatazo?

A. Walimpenda
B. Walimhurumia
C. Walimtenga
D. Walimhusudu
E. Walimchekesha

**Jedwali Na. 2.3: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 54,843 | 96,437 | 671,839 | 57,933 | 24,813 | 11,221 |
| Asilimia ya watahiniwa | 5.98 | 10.52 | 73.26 | 6.32 | 2.71 | 1.22 |

Swali lillenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu maana na matumizi ya msamiati wa lugha ya Kiswahili. Kiwango cha kufaulu kwa wataniniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kama **Jedwali 2.3** linavyodhihirisha mtawanyo wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo. Watahiniwa 671,839 (73.26%) waliweza kuchagua jibu sahihi *C Walimtenga*. Watahiniwa hao wameonesha kuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu maana ya neno 'nyanyapaa' kuwa ni kumtenga mtu kutokana na hali yake ya kiafya, imani, tabaka au kabila. Hata hivyo, uchaguzi wa jibu hili umechangiwa na matumizi makubwa ya neno *nyanyapaa* ambalo lina uhalisia zaidi kutokana na janga la ugonjwa wa UKIMWI ambapo baadhi ya waathirika wamekuwa wakitengwa katika jamii zao.

Watahiniwa wachache, asilimia 25.52 walichagua vipotoshi *A Walimpenda, B Walimhurumia, D Walimhusudu na E Walimchekesha.* Watahiniwa waliochagua *A, Walimpenda* hawakuwa wanajua maana ya neno hilo kuwa ni hali ya mtu kuvutiwa na mtu kutokana na ubora

au uzuri wake, hivyo mtu hawezi kumnyanyapaa mtu anayemuona kuwa ni bora. Aidha, watahiniwa waliochagua *B Walimhurumia* hawakutambua neno hilo huonesha hisia ya kumsaidia mtu mwenye shida. Hali kadhalika, uchaguzi *D, Walimhusudu* lina maana ya kuona wivu dhidi ya mtu mwingine, na *E Walimchekesha* lilikuwa na maana ya kuanzisha kicheko chenye kufanya watu wengine kucheka; maana ambazo hazihusiani kabisa na hali ya kunyanyapaa au kumtenga mtu. Uteuzi wa vipotoshi hivyo unaonesha wazi kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana za misamiati ya lugha ya Kiswahili.


**Swali la 12**: Neno “nimerudi” lipo katika nafsi ipi?

A. Pili umoja
B. Kwanza umoja
C. Kwanza wingi
D. Tatu umoja
E. Tatu wingi

Swali lilikuwa linapima ujuzi wa mtahiniwa katika matumizi ya nafsi kwenye vitenzi vya Kiswahili. Swali hili lilikuwa na kiwango kizuri cha kufaulu ambapo watahiniwa 612,666 sawa na asilimia 66.81 walichagua jibu sahihi *B Kwanza umoja*. Watahiniwa hao wameonesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maumbo yanayowakilisha nafsi katika vitenzi vya Kiswahili. Vile vile, watahiniwa hao wana uelewa wa kutosha kuhusu nafsi mbalimbali katika lugha ya Kiswahili yaani nafsi ya kwanza, nafsi ya pili na nafsi ya tatu katika umoja na wingi.

Baadhi ya watahiniwa kiasi cha asilimia 31.9 walioshindwa kujibu swali hili walichagua vipotoshi *A Pili umoja, C Kwanza wingi, D Tatu umoja na E Tatu wingi*. Miongoni mwa watahiniwa hao, asilimia

(13.11%) sawa na watahiniwa 120,195 walichagua *A, Pili umoja* kutokana na kukosa maarifa kuhusu nafsi ya pili umoja inayowakilishwa kwa umbo **u-**. Watahiniwa hao walivutiwa na umbo **ni-** ambalo ni umbo la umoja katika nafsi ya kwanza. Watahiniwa waliochagua *C, Kwanza wingi* hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maumbo yanayowakilisha nafsi katika hali ya umoja na wingi kwa kuwa nafsi pekee iliyopo katika neno "nimerudi" ni umoja. Uteuzi wa *D, Tatu umoja* na *E, Tatu wingi* unaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu nafsi ya tatu umoja yenye umbo (a-) na wingi (wa-) kwenye vitenzi ya Kiswahili. Kwa jumla, uteuzi wa vipotoshi hivyo unadhihirisha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maumbo yanayowakilisha nafsi katika vitenzi vya Kiswahili. **Kielelezo 2.8** kinaonesha mtawanyo wa majibu ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Kielelezo 2.8** *kinaonesha kiwango kizuri cha kufaulu kwa watahiniwa ambapo asilimia 66.81 waliweza kutaja kwa usahihi nafsi katika neno* 'nimerudi' *kuwa ni kwanza umoja.*

**Swali la 13**: “Kiwanda hutoa ajira kwa wananchi.” Kiwanda ni aina gani ya neno?

A. Kivumishi
B. Kiwakilishi
C. Nomino
D. Kielezi
E. Kitenzi

**Jedwali 2.4: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 49,942 | 86,630 | 642,177 | 88,141 | 39,289 | 10,907 |
| Asilimia ya watahiniwa | 5.45 | 9.45 | 70.02 | 9.61 | 4.28 | 1.19 |

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa wa kutambua aina za maneno kama yalivyotumika katika sentensi. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa ni kizuri ambapo watahiniwa 642,177 sawa na asilimia 70.02 waliweza kuchagua jibu sahihi *C Nomino*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu aina za maneno na kuweza kutambua mkao wa aina mbalimbali za maneno katika sentensi. Mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo umeoneshwa katika **Jedwali 2.4**.

Watahiniwa wengine, jumla ya asilimia 28.79 walichagua vipotoshi *A Kivumishi, B Kiwakilishi, D Kielezi na E Kitenzi* ili kuonesha aina ya neno ‘kiwanda’ katika sentensi waliyopewa. Watahiniwa hao walishindwa kubaini neno hilo kwa usahihi kutokana na kutozingatia mkao wa maneno katika sentensi husika. Aidha, uteuzi wa *A, Kivumishi* unaonesha watahiniwa kukosa maarifa kwani kivumishi ni neno linalofafanua nomino, *B Kiwakilishi* walishindwa kutambua kuwa ni neno linalosimama badala ya jina au kitu, wakati *D Kielezi* ni neno linalotoa maelezo zaidi kuhusu kitenzi. Mwisho, uteuzi wa *E Kitenzi*,

watahiniwa hawakutambua kuwa ni neno linaloeleza au linalohusu tendo. Kwa jumla, neno 'kiwanda' halina uhusiano wowote na aina hizo za maneno. Hivyo, uteuzi wa vipotoshi hivyo unadhihirisha kuwa watahiniwa hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu aina za maneno hususan nomino.

**Swali la 14**: "Mashine nyingi hupatikana kiwandani." "Kiwandani' ni aina gani ya neno?

A. Kivumishi
B. Kiwakilishi
C. Nomino
D. Kielezi
E. Kitenzi.

**Jedwali 2.5: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 71,140 | 102,452 | 192,562 | 476,956 | 62,307 | 11,669 |
| Asilimia ya watahiniwa | 7.76 | 11.17 | 21.00 | 52.01 | 6.79 | 1.27 |

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa wa kutambua aina za maneno kama yalivyotumika katika sentensi. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa ni cha wastani. Mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa katika asilimia umeoneshwa katika **Jedwali 2.5**. Watahiniwa 476,956 sawa na asilimia 52.01 waliweza kuchagua jibu sahihi *D Kielezi*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu aina za maneno na jinsi yanavyobainishwa katika sentensi. Aidha, watahiniwa walikuwa na uelewa wa dhana ya kuongeza **–ni** mwishoni mwa baadhi ya nomino ili kuunda vielezi vya mahali.

Watahiniwa wengine ambao ni asilimia 46.8 walichagua *vipotoshi A Kivumishi, B Kiwakilishi, C Nomino na E Kitenzi*. Idadi kubwa ya

watahiniwa (21.00%) walichagua *C, Nomino* kwa kuwa neno 'kiwandani' limetokana na nyongeza ya umbo (–ni) katika nomino 'kiwanda' na hivyo kuvutiwa zaidi na kipotoshi hicho kuwa ni nomino. Aidha, watahiniwa wengine walishindwa kubaini aina za maneno kwa kuzingatia mpangilio wa maneno hayo katika sentensi. Watahiniwa waliochagua vipotoshi *A Kivumishi, B Kiwakilishi* na *E Kitenzi* hawakujua maana za maneno hayo kuwa:

> *kivumishi* ni neno linalofafanua nomino; *kiwakilishi* ni neno linalosimama badala ya jina (nomino) au kitu na kitenzi ni aina ya neno linaloeleza tendo.

Mchanganuo huo unaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu aina za maneno hususan kielezi na utokeaji wake katika sentensi.

**Swali la 15**: Kisawe cha neno "ndovu" ni kipi kati ya maneno yafuatayo?

A. Nyati
B. Faru
C. Nyumbu
D. Tembo
E. Mbogo

**Jedwali 2.6: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 99,096 | 95,317 | 49,244 | 613,518 | 48,219 | 11,692 |
| Asilimia ya watahiniwa | 10.81 | 10.39 | 5.37 | 66.90 | 5.26 | 1.27 |

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu matumizi ya maneno yenye mfanano. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa ni kizuri. **Jedwali 2.6** linaonesha asilimia ya majibu kwa watahiniwa katika kila chaguo. Watahiniwa 613,518 sawa na

asilimia 66.90 waliweza kuchagua jibu sahihi *D Tembo* kwa kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu uhusiano wa msamiati *ndovu* na *tembo* ambapo:

> Ndovu ni mnyamapori ambaye ni mkubwa sana, mwenye mkonga mrefu, pembe nyeupe na masikio mapana. Jina lingine la mnyama huyo ni tembo.

Licha ya kiwango cha wastani cha kufaulu, asilimia 31.83 ya watahiniwa walishindwa kubaini kisawe cha neno 'ndovu' kwa kuchagua vipotoshi *A Nyati, B Faru, C Nyumbu na E Mbogo.* Watahiniwa walishindwa kutambua kuwa wanyama walio katika vipotoshi hivyo wana tofauti kati ya mmoja na mwingine ambapo;

> *Nyati* ni mnyama mkubwa wa nchi kavu, jamii ya ng'ombe mwenye pembe zilizopinda kuelekea juu. *Faru* ni mnyama mwenye umbo kubwa anayefanana na kiboko; *nyumbu* ni mnyamapori jamii ya ng'ombe ambaye ana miguu mirefu ya mbele kuliko ya nyuma, mkia mrefu na shingo yenye manyoya mengi mtawalia na *mbogo* ni mnyama mkubwa wa porini mithili ya ng'ombe mwenye pembe kubwa zilizokunjika mbele.

Hivyo, uteuzi wa vipotoshi hivyo unadhihirisha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu majina mbalimbali ya wanyama hasa wale walio katika kundi moja na hivyo kushindwa kubaini kuwa jina lingine la 'ndovu' ni tembo.

**Swali la 16**: "Mlima Meru unafuka moshi." Ukanushi wa sentensi hii ni upi?

A. Mlima Meru unawaka moshi
B. Mlima Meru unatoa moshi
C. Mlima Meru unafukiza moshi
D. Mlima Meru haufuki moshi
E. Mlima Meru hauwaki moshi

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu ukanushi katika sentensi. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili

kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 577,040 sawa na asilimia 62.92 waliweza kuchagua jibu sahihi *D Mlima Meru haufuki moshi*. Watahiniwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maumbo ya ukanushi katika vitenzi ambayo huwakilishwa na umbo **ha-** linaloambatana na kitenzi.

Pamoja na kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa kuwa kizuri, asilimia 35.92 ya watahiniwa walishindwa kubaini ukanushi katika sentensi kwa kuchagua vipotoshi *A Mlima Meru unawaka moshi, B Mlima Meru unatoa moshi, C Mlima Meru unafukiza moshi* na *E Mlima Meru hauwaki moshi*. Miongoni mwao, watahiniwa 195,102 (21.27%) waliteua *B Mlima Meru unatoa moshi*, kipotoshi kilichowavutia watahiniwa wengi zaidi kutokana na neno ‘kutoa’ waliloshabihisha na ‘kufuka’ ambalo ni kisawe chake badala ya kuonesha ukanushi wa sentensi hiyo. Aidha, watahiniwa waliochagua *A,* (4.2%) *C*, (6.5%) na *E* (3.9%), uteuzi wao unadhihirisha kuwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maumbo yanayowakilisha ukanushi katika vitenzi.

**Swali la 17**: Panga maneno yafuatayo kwa kuanzia na neno ambalo katika familia hiyo linaonesha aliyetangulia kuzaliwa hadi wa mwisho kuzaliwa: Baba, kitukuu, babu, kilembwe, mjukuu, kilembwekeza


A. Babu, baba, mjukuu, kitukuu, kilembwe, kilembwekeza
B. Baba, mjukuu, kitukuu, kilembwe, kilembwekeza, babu
C. Kilembwekeza, kitukuu, mjukuu, baba, babu, kilembwe
D. Babu, mjukuu, kitukuu, kilembwe, kilembwekeza,baba
E. Mjukuu, kitukuu, baba, babu, kilembwe, kilembwekeza

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kuweka mpangilio sahihi wa maneno kwa kuzingatia uhusiano wa mti wa ukoo. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri. Watahiniwa 749,220 sawa na asilimia 81.70 waliweza kuchagua jibu sahihi *A Babu, baba, mjukuu, kitukuu, kilembwe, kilembwekeza* kutokana na uelewa wao kuhusu ngazi ya uzao katika mti wa ukoo.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 157,215 (17.2%) walishindwa kubaini mpangilio na uhusiano wa wanandugu katika mti wa ukoo na kuchagua vipotoshi *B Baba, mjukuu, kitukuu, kilembwe, kilembwekeza, babu, C Kilembwekeza, kitukuu, mjukuu, baba, babu, kilembwe, D Babu, mjukuu, kitukuu, kilembwe, kilembwekeza, baba na E Mjukuu, kitukuu, baba, babu, kilembwe, kilembwekeza*. Watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuelewa kuwa:

> baba ni mzazi wa kiume, babu ni baba mzazi wa baba au mama, mjukuu ni mtoto wa mwanao wa kike au wa kiume, kitukuu ni mtoto wa mjukuu, kilembwe ni mtoto anayezaliwa na mjukuu na kilembwekeza ni mtoto ambaye mzazi wake ni kilembwe.

Hivyo, uteuzi wa vipotoshi B, C, D na E unaonesha kwamba watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mti wa ukoo. **Kielelezo 2.9** kinaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.




**Kielelezo 2.9** *kinaonesha kiwango kizuri cha kufaulu ambapo watahiniwa wengi, asilimia 80.70, waliweza kupanga maneno katika familia kwa kuonesha aliyetangulia kuzaliwa hadi wa mwisho kuzaliwa katika mti wa ukoo.*

**Swali la 18:** Kisawe cha neno "kinying'inya" ni kipi katika maneno yafuatayo?

A. Mjukuu
B. Kitukuu
C. Kijukuu
D. Kilembwe
E. Kilembwekeza

**Jedwali 2.7: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 86,847 | 191,272 | 89,798 | 126,130 | 408,891 | 14,148 |
| Asilimia ya watahiniwa | 9.47 | 20.86 | 9.79 | 13.75 | 44.59 | 1.54 |

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika matumizi ya maneno yenye mfanano. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani. Mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa

umeoneshwa katika **Jedwali 2.7**. Idadi kubwa ya watahiniwa (53.87%) walishindwa kubaini kisawe cha neno 'kinying'inya' kwa kuchagua vipotoshi *A Mjukuu, B kitukuu, C Kijukuu na D* Kilembwe. Watahiniwa hao walishindwa kutambua kuwa Kinying'inya hushabihiana na Kilembwekeza. Kwa jumla, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya neno moja linaloweza kuwasilishwa na maneno tofauti katika lugha ya Kiswahili.


Watahiniwa 408,891 sawa na asilimia 44.6 waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni *E Kilembwekeza*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya msamiati 'kinying'inya' ambao unashabihiana na kilembwekeza. Kinying'inya/kilembwekeza ni mtoto ambaye mzazi wake ni kilembwe au ni mtoto wa kilembwe. Hivyo, kinying'inya ni kisawe cha kilembwekeza kwa kuwa zote zina maana sawa.

**Swali la 19:** Kisawe cha neno "mviringo" ni kipi?

A. Bapa
B. Duara
C. Mstatili
D. Pembe tatu
E. Pembe nne

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika matumizi ya maneno yenye mfanano. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri. Watahiniwa 813,725 sawa na asilimia 88.73 waliweza kuchagua jibu sahihi *B Duara*. Watahiniwa waliochagua jibu hilo walikuwa na maarifa ya kutosha kuwa neno mviringo linashabihiana na msamiati duara. Hivyo inadhihirisha kuwa, watahiniwa hao wana uelewa kuhusu maneno zaidi ya moja yenye maana sawa (visawe) vilivyopo katika lugha ya Kiswahili.

Watahiniwa wachache asilimia 10.21 walishindwa kubaini kisawe cha neno 'mviringo' hivyo wakachagua vipotoshi *A Bapa, C Mstatili, D Pembetatu na E Pembe nne*. Uteuzi wa vipotoshi *A bapa* inahusu umbo la ulalo, *C mstatili* na *E Pembe nne,* yote ni maumbo yenye pande nne, na *D Pembetatu* huhusisha umbo lenye mistari mitatu inayokutana kwenye ncha. Maneno yaliyopo katika vipotoshi hivyo hayana mfanano wowote na umbo la mviringo yaani duara. Uteuzi huu unadhihirisha kuwa watahiniwa hawana uelewa kuhusu maneno zaidi ya moja yenye maana sawa (visawe) yaliyopo katika lugha ya Kiswahili. **Kielelezo 2.10** kinaonesha asilimia ya majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.




**Kielelezo 2.10** *kinaonesha kiwango kizuri cha kufaulu ambapo watahiniwa wengi, asilimia 88.73, waliweza kubaini kisawe cha neno 'mviringo' kuwa ni duara.*

**Swali la 20**: Mtu anayechonga vinyago anaitwaje?

A. Mnajimu
B. Boharia
C. Msanii
D. Mwashi
E. Seremala

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu maana na matumizi ya msamiati. Swali hili lilikuwa na kiwango hafifu cha kufaulu. Idadi kubwa ya watahiniwa (669,356), sawa na asilimia 72.99, walishindwa kujibu swali kwa usahihi kutokana na kuchagua vipotoshi *A Mnajimu, B Boharia, D Mwashi* na *E Seremala*. Watahiniwa hao hawakuweza kutaja jina la mtu anayechonga vinyago. Aidha hawakuwa na maarifa ya kutofautisha maana ya neno moja na lingine katika machaguo waliyopewa. Uteuzi wa *A, Mnajimu* (11.75%) ambaye ni mtu mwenye elimu ya Sayansi ya utafiti na ugunduzi wa mambo ya anga za juu na uchaguzi wa *B Boharia* (24.39%), ambaye ni mtu anayetunza bidhaa zilizomo katika bohari; hazina uhusiano wowote na mchongaji wa vinyago. Aidha, watahiniwa wengi (245,883), sawa na asilimia 26.81, walichagua kipotoshi *E Seremala* ambaye ni fundi anayetengeneza samani, Walivutiwa na jibu hilo zaidi kwa kuwa seremala hutumia mbao ili kutengeneza vifaa mbalimbali na hivyo walishabihisha kazi hiyo na kuchonga vinyago bila kutambua kuwa ni kazi tofauti. Watahiniwa wachache (92,037), sawa na asilimia 10.04 walichagua kipotoshi *D, Mwashi* ambaye ni mtu anayetumia ujuzi wa kujenga nyumba kwa kutumia mawe au tofali lakini hachongi vinyago. Watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo, hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kazi ya kuchonga vinyago ambayo hufanywa na *msanii* mwenye ujuzi na ubunifu wa kutengeneza picha yenye kubeba ujumbe maalum kwa wahusika wanaolengwa kwenye kinyago hicho.

Watahiniwa wengine asilimia 25.4 waliweza kuchagua jibu sahihi *C Msanii.* Uteuzi wa jibu hilo unaonesha kuwa watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya msanii ambaye ni mtu aliye na ujuzi wa kuchonga au kuchora mfano wa kitu au mtu kwa kutumia ujuzi na ubunifu.

## 2.2 Sehemu B: Lugha ya Kifasihi


**Swali la 21:** Alipomwona yule chui, Juma akapiga moyo konde na kuanza kumshambulia kwa mpini wa jembe. Maana ya msemo kupiga moyo konde ni ipi?

A. Kujikaza
B. Kuamua
C. Kutetemeka
D. Kutaharuki
E. Kuruka

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kutambua misemo katika lugha ya kifasihi hasa nahau. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri. Watahiniwa 645,487 sawa na asilimia 70.38 waliweza kuchagua jibu sahihi *A Kujikaza*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya maneno na matumizi yake, hivyo waliweza kubaini kuwa *kupiga moyo konde* ni kujikaza yaani kujitahidi au kuwa imara katika kufanya jambo fulani.

Watahiniwa wengine 260,400 sawa na asilimia 28.40 walichagua vipotoshi *B Kuamua, C Kutetemeka, D Kutaharuki na E Kuruka* kutokana na kukosa uelewa kuhusu maana ya nahau katika lugha ya Kiswahili. Watahiniwa wengi (14.91%) walivutiwa na kipotoshi *B, Kuamua,* neno ambalo lina maana ya kukata shauri kuhusu jambo fulani. Watahiniwa hao walishindwa kutafakari kuwa kuamua ni hatua inayofuata baada ya mtu kufanya jitihada ya kutaka kutekeleza jambo fulani. Kwa jumla, uteuzi wa vipotoshi vingine vyote unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana na matumizi ya misamiati iliyopo katika vipotoshi hivyo. Kwa mfano, *C Kutetemeka* ni neno lenye maana ya kutikisika kwa mwili kutokana na woga au kuhisi baridi kali, *D Kutaharuki* lina maana ya kuingiwa na wasiwasi au hofu na *E Kuruka* lina maana ya kukataa kukiri jambo

unalolijua, kupinga au kubisha kuhusu jambo fulani; maana ambazo haziendani na hali ya 'kupiga moyo konde' yaani kuonyesha ushupavu wa kufanya jambo au kugangamala (kujikaza). **Kielelezo Na. 2.11** kinaonesha asilimia ya majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.




**Kielelezo 2.11** *kinaonesha kiwango kizuri cha kufaulu ambapo watahiniwa wengi, asilimia 70.38, waliweza kueleza maana ya nahau kupiga moyo konde yaani 'kujikaza'*.

**Swali la 22:** Nimeugua kwa kipindi kirefu sana, lakini sasa ni ______________wa afya. Neno lipi linakamilisha sentensi hii?

A. hoi
B. buheri
C. buheli
D. mzuri
E. mwingi

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu matumizi ya msamiati katika lugha ya Kiswahili. Kiwango cha kufaulu kwa

watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani. Watahiniwa 523,682 sawa na asilimia 57.10 waliweza kuchagua jibu sahihi *B Buheri* lenye maana ya hali ya kuwa salama au utulivu. Uchaguzi sahihi wa jibu hili unadhihirisha kuwa watahiniwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu misamiati mbalimbali ya lugha ya Kiswahili.

Hata hivyo, watahiniwa 381,709 (41.62%) walichagua vipotoshi *A Hoi, C Buheli D Mzuri na E Mwingi.* Watahiniwa 37,348 (4.7%) walichagua kipotoshi *A Hoi,* kwa kuwa hawakuwa na uelewa wa neno hilo ambalo ni sawa na kuugua sana*.* Uteuzi wa *C Buheli* ulifanywa na (15.40%) ya watahiniwa waliojibu swali hili, hawakutambua kwamba neno hilo sio sanifu kwa sababu ya kosa la kisarufi la silabi 'li'ambapo usahihi wa neno hilo ni buhe<u>ri</u>, jambo linaloashiria kuwa watahiniwa hao wana athari ya lugha mama, hivyo kushindwa kutambua kosa hilo la kimatamshi. Aidha, watahiniwa (18.38%) walichagua kipotoshi *D, Mzuri* chenye maana ya sifa anayopewa mtu, na idadi ndogo (3.77%) waliochagua *E, Mwingi (wingi wa kitu au vitu)*, hawakujua kuwa maneno hayo hayahusiani na muktadha wa sentensi hiyo yenye kuonesha hali ya mtu kupata nafuu katika ugonjwa. Hata hivyo asilimia 1.28 ya watahiniwa hawakujibu swali hili na miongoni mwao walitoa jibu zaidi ya moja. Kwa jumla, uteuzi wa vipotoshi A, C, D na E unaonesha kuwa watahiniwa hao hawana ujuzi wa kutosha kuhusu msamiati wa lugha ya Kiswahili.

**Swali la 23:** Wakikua mama yao huwatupa mbali kwa kishindo. Jibu la kitendawili hiki ni lipi?

A. Mbarika

B. Nazi

C. Mahindi

D. Embe

E. Mtama

**Jedwali 2.8: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 482,888 | 210,172 | 47,428 | 131,755 | 32,690 | 12,153 |
| Asilimia ya watahiniwa | 52.65 | 22.92 | 5.17 | 14.37 | 3.56 | 1.33 |

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu matumizi na uteguzi wa vitendawili. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani kama kilivyooneshwa katika **Jedwali 2.8.** Watahiniwa 482,888 sawa na asilimia 52.7 waliweza kuchagua jibu sahihi *A Mbarika*, chaguo ambalo linategua kitendawili 'wakikua mama yao huwatupa mbali kwa kishindo'. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya mbarika kuwa ni mbegu za mnyonyo ambazo hutoa mafuta yanayotumika kama dawa ambapo zinapokomaa kwenye mti, kokwa lake hupasuka na kuzirusha mbali.

Watahiniwa wengine asilimia 46.1 walichagua vipotoshi *B Nazi C Mahindi D Embe na E Mtama*. Miongoni mwao, karibia nusu ya watahiniwa (22.92%) walivutiwa na kipotoshi *B, Nazi* kwa kuwa hawakuelewa kuwa mara nyingi nazi huanguliwa na mkwezi hivyo ni mara chache hudondoka. Aidha, nazi huweza kuanguliwa kabla ya kukomaa na kutumika kama dafu yaani nazi changa. Uteuzi wa vipotoshi *C Mahindi na E Mtama* ulitokana na watahiniwa hao kufananisha tendo la kupukuchuliwa kwa mahindi/mtama na tendo la kutupwa mbali kwa mbarika. Aidha, uteuzi wa kipotoshi *D, Embe* kumetokana na kushabihisha mwanguko wa embe zinapokomaa na na hali ya kutupwa mbali kwa mbarika japokuwa hakuna mfanano wowote kwa kuwa embe hudondokea chini ya mti wake na hazitupwi mbali kama mbarika. Kwa jumla, uteuzi wa vipotoshi hivyo

unadhihirisha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu msamiati wa Lugha ya Kiswahili.

**Swali la 24:** Kati ya methali zifuatazo ni ipi **haitoi** msisitizo wa kufanya juhudi katika jambo?

A. Maji ukiyavulia nguo sharti uyaoge
B. Bandu bandu humaliza gogo
C. Mwenda bure si mkaa bure huenda akaokota
D. Panapofuka moshi hapakosi moto
E. Ukupigao ndio ukufunzao

**Jedwali 2.9: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 136,684 | 304,019 | 164,309 | 131,934 | 165,923 | 14,217 |
| Asilimia ya watahiniwa | 14.90 | 33.15 | 17.92 | 14.39 | 18.09 | 1.55 |

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kubaini maana na matumizi ya methali za Kiswahili. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa kilikuwa hafifu. Kwa jumla, mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa hakuna tofauti kubwa kati ya majibu sahihi na vipotoshi kama **Jedwali. 2.9** linavyodhihirisha. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa kiwango hafifu zaidi cha kufaulu. Watahiniwa wengi, 770,935 sawa na asilimia 84.06, walichagua vipotoshi *A Maji ukiyavulia nguo sharti uyaoge*, *B Bandu bandu humaliza gogo, C Mwenda bure si mkaa bure huenda akaokota na E Ukupigao ndio ukufunzao*. Miongoni mwao, watahiniwa wengi 304,019 (33.2%) walichagua kipotoshi *B Bandu bandu humaliza gogo* kwa kudhani kuwa methali hiyo haitoi msisitizo wa jambo wakati

methali hiyo huhimiza ufanyikaji wa jambo kwa namna ya taratibu/juhudi ndogo na hatimaye jambo hilo hukamilika. Kwa jumla, uteuzi wa vipotoshi vingine ambavyo vilikuwa na methali zenye msisitizo wa kufanya jambo kunadhihirisha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana na matumizi ya methali hizo.

Watahiniwa wachache, 131,934 sawa na asilimia 14.39 ndio walioweza kuchagua jibu sahihi, *D Panapofuka moshi hapakosi moto*, methali isiyokuwa na msisitizo wa kufanya jambo bali huonesha tu dalili/ishara za jambo kutukia. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana na matumizi ya methali hiyo.


**Swali la 25**: "Kutoa ni moyo usambe ni utajiri." Maana ya methali hii ni ipi?

A. Matajiri ndio wenye moyo wa kutoa.
B. Maskini ndio wenye moyo wa kusaidia.
C. Kuonyesha moyo wa ukarimu hakuhitaji utajiri.
D. Umaskini na utajiri havitangamani.
E. Mwenye nacho ni tajiri.

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kubaini maana na matumizi ya methali za Kiswahili. Takwimu zinaonesha kuwa kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri**.** Watahiniwa 634,410 sawa na asilimia 69.18 waliweza kuchagua jibu sahihi *C Kuonyesha moyo wa ukarimu hakuhitaji utajiri.* Hivyo, inaonesha kuwa watahiniwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana na matumizi ya methali mbalimbali na walielewa kuwa si lazima mtu awe na utajiri ndipo atoe msaada, ila jambo la msingi ni moyo wa utoaji.

Watahiniwa 271,049 sawa na asilimia 29.55 walichagua vipotoshi *A, Matajiri ndio wenye moyo wa kutoa*, *B Maskini ndio wenye moyo wa*

*kusaidia*, *D Umaskini na utajiri havitangamani* na *E Mwenye nacho ni tajiri*. Watahiniwa waliochagua vipotoshi *A, Matajiri ndio wenye moyo wa kutoa* walikuwa na ufahamu kulingana na mazingira yao kuwa matajiri ndio wenye fedha nyingi na hutoa misaada kwa maskini. Aidha, watahiniwa waliochagua kipotoshi *B Maskini ndio wenye moyo wa kusaidia* walivutiwa na jibu hilo ambalo linaonesha japokuwa maskini hana kitu lakini yuko mstari wa mbele katika kusaidia wengine. Uteuzi wa kipotoshi *D Umaskini na utajiri havitangamani* ulitokana na uelewa wa watahiniwa kuwa maskini na tajiri hawawezi kushirikiana kutokana na tofauti za vipato vyao. Mwisho, uteuzi wa kipotoshi *E Mwenye nacho ni tajiri* ulivutiwa na watahiniwa kwani wanajua kuwa tajiri ndiye mwenye fedha na kila kitu kizuri. Uteuzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa walishindwa kubaini maana na matumizi ya methali za Kiswahili. Mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo umeoneshwa katika **Kielelezo 2.12.**




**Kielelezo 2.12:** *Kinaonesha kiwango kizuri cha kufaulu ambapo asilimia 69.18 ya watahiniwa waliweza kubaini maana ya methali 'kutoa ni moyo usambe ni utajiri' ambayo ni 'kuonyesha* moyo wa ukarimu hakuhitaji utajiri'*.*

**Swali la 26:** "____________________ sihimili kishindo." Kifungu kipi cha maneno kinakamilisha methali hii?

A. Mimi nyumba ya nyasi
B. Mimi nyumba ya miti
C. Mimi nyumba ya vioo
D. Mimi nyumba ya udongo
E. Mimi nyumba ya zamani

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua kifungu cha maneno kinachokamilisha methali waliyopewa. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani ambapo watahiniwa 451,937 sawa na asilimia 49.28 waliweza kuchagua jibu sahihi *D Mimi nyumba ya udongo*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa kuwa nyumba inayojengwa kwa udongo sio imara kwani ikinyeshewa na mvua udongo wake huporomoka.

Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa 451,165 sawa na asilimia 49.28 walichagua vipotoshi *A Mimi nyumba ya nyasi* (18.18%), B *Mimi nyumba ya miti* (8.12%), *C Mimi nyumba ya vioo* (10.74%) na E *Mimi nyumba ya zamani* (12.16%). Watahiniwa waliochagua kipotoshi *A, Mimi nyumba ya nyasi* walishindwa kuelewa kuwa nyumba ya nyasi inaweza kuhimili vishindo vya mvua, upepo isipokuwa moto. Aidha, watahiniwa waliochagua kipotoshi B *Mimi nyumba ya miti* walielewa kuwa nyumba ya udongo hujengwa kwa kutumia miti, *C Mimi nyumba ya vioo* inaonesha hawana uelewa kabisa kuhusu nyumba za udongo, bali wana uelewa kuhusu nyumba zenye madirisha ya vioo, hivyo wakavutiwa na jibu hilo. Hata hivyo waliochagua vipotoshi hivyo hawakutafakari kuwa dhana ya 'sihimili kishindo' ni kutoweza kukabiliana na sauti yenye mtetemo inayosikika baada ya kitu kizito kudondoka. Hivyo, uteuzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu muundo na

maana ya methali za Kiswahili. Hata hivyo uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 13,984 (1.52%) walichagua jibu zaidi ya moja na wengine hawakuchagua jibu lolote.


**Swali la 27:** "Asiyeuliza ___________." Maneno yapi yanakamilisha methali hii kwa usahihi?

A. kaa naye mbali
B. hana budi kujua
C. usimwambie kitu
D. usimuulize lolote
E. hana ajifunzalo

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua muundo na maana ya methali za Kiswahili. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri na watahiniwa. Watahiniwa 741,500 sawa na asilimia 80.85 waliweza kuchagua jibu sahihi *E hana ajifunzalo* kwa sababu walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana, muundo na matumizi ya methali za Kiswahili.

Hata hivyo, idadi ya watahiniwa 163,749 sawa na asilimia 17.85, walichagua vipotoshi *A kaa naye mbali, B hana budi kujua, C usimwambie kitu* na *D usimuulize lolote.* Uteuzi wa kipotoshi *A, kaa naye mbali* kiliwavutia watahiniwa kuona kuwa mtu asiyeuliza kitu asichokijua iwapo utakaa naye karibu atakufanya usijue kitu. Aidha, waliochagua kipotoshi *B hana budi kujua* walivutiwa na jibu hilo kwa kuwa mtu asiyejua jambo huambiwa ili ajue. Vilevile uchaguzi wa kipotoshi *C usimwambie kitu* walielewa kuwa mtu asiyejua jambo hastahili kuambiwa. Kipotoshi *D "usimuulize lolote* walielewa kuwa mtu asiyeuliza kitu asiulizwe chochote. Uteuzi wa vipotoshi hivyo unadhihirisha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu maana, muundo na matumizi ya methali katika lugha ya

Kiswahili. **Kielelezo 2.13** kinaonesha asilimia ya majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.




**Kielelezo 2.13:** *Kinaonesha kiwango kizuri cha kufaulu ambapo asilimia 69.18 ya watahiniwa waliweza kukamilisha methali Asiyeuliza 'hana ajifunzalo'.*

**Swali la 28:** "Gari langu halitumii mafuta". Jibu la kitendawili hiki ni lipi?

A. Macho
B. Miguu
C. Mikono
D. Tumbo
E. Masikio

**Jedwali 2.10: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 22,684 | 822,852 | 21,455 | 23,549 | 16,322 | 10,224 |
| Asilimia ya watahiniwa | 2.47 | 89.72 | 2.34 | 2.57 | 1.78 | 1.11 |

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika matumizi na uteguzi wa vitendawili. Mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa umeoneshwa katika **Jedwali 2.10.** Takwimu za kiwango cha kufaulu zinaonesha kuwa, swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri na watahiniwa wengi. Idadi ya watahiniwa waliochagua jibu sahihi ni 822,852 sawa na asilimia 89.72. Watahiniwa hao waliweza kubaini jibu *B Miguu* inayohusiana na dhana ya gari yaani chombo kinachotumia mafuta ili kiweze kutembea. Hivyo, katika kutegua kitendawili hicho, watahiniwa hao walitoa jibu sahihi “miguu” ambayo ni viungo vya mwili vinavyoweza kutembea kama gari bila kutumia mafuta.

Aidha, jumla ya watahiniwa 84,010 sawa na asilimia 9.16 walichagua vipotoshi *A Macho, C Mikono, D Tumbo* na *E Masikio*. Vipotoshi hivyo vinahusisha viungo vya mwili wa binadamu lakini haviwezi kujitegemea ili kutembea kutoka sehemu moja kwenda nyingine kama miguu inavyoweza kufanya. Vipotoshi hivyo vinahusisha viungo vya mwili vyenye kazi tofauti:

> Macho yana kazi ya kuona, mikono kushika kitu, tumbo kwa ajili ya kusaga chakula na masikio kwa ajili ya kusikia.

Hivyo, viungo hivyo ni muhimu katika mwili wa binadamu lakini haviwezi kutembea kama miguu inavyofanya. Aidha, inadhihirisha watahiniwa hawa walishindwa kushabihisha uwezo wa gari wa kutembea kwa kila kipotoshi.

**Swali la 29**: “Anatengeneza mchuzi mtamu sana lakini hapiki jikoni.”

Kitendawili hiki jibu lake ni lipi?

A. Ng’ombe
B. Nyuki
C. Mbuzi

D. Muwa
E. Mbuzi

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu maana na matumizi ya msamiati katika kutegua kitendawili. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri. Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 632,325 sawa na asilimia 68.9 waliweza kuchagua jibu sahihi *B Nyuki*. Watahiniwa walichagua jibu hilo kwa kuwa walikuwa na uelewa kuwa nyuki ni mdudu ambaye hutengeneza asali ambayo imefananishwa na mchuzi mtamu kutokana na utamu wa asali. Aidha, uteuzi huo ulitokana na maarifa waliyonayo katika somo la Sayansi kuhusu nyuki.

Hata hivyo, jumla ya watahiniwa 273,669 (29.9%) walichagua vipotoshi *A Ng'ombe* 30,948 (3.40%), *C Mbuzi* 27,553 (3.00%), *D Muwa* 202,308 (22.10%) na *E Mbuzi* 12,860 (1.40%). Watahiniwa waliochagua vipotoshi *Ng'ombe*, *C Mbuzi*, na *E Mbuzi* walivutiwa na majibu hayo kwa kuwa wote ni wanyama wanaotoa maziwa ambayo ni vimiminika kama mchuzi lakini hayana sukari. Uteuzi wa kipotoshi *D Muwa*, uliwavutia watahiniwa kwa kuwa 'muwa' ni zao linalotoa kimimika chenye sukari. Kwa jumla, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo walishindwa kuhusisha majibu yao na nyuki anayetengeneza asali. Aidha, watahiniwa 11,092 (1.20%) walichagua jibu zaidi ya moja na wengine hawakuchagua jibu lolote.

**Swali la 30**: "Ukiona vyaelea vimeundwa." Methali hii ina maana gani?

A. Ubora wa kitu hautegemei upya wake
B. Vitu vinavyoelea baharini ni meli
C. Vitu vya thamani hupatikana kwa jasho
D. Vitu vimeumbwa ili vielee
E. Vitu vya thamani vimeundwa

**Jedwali 2.11: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 287,377 | 50,716 | 471,027 | 37,371 | 57,721 | 12,874 |
| Asilimia ya watahiniwa | 31.30 | 5.50 | 51.40 | 4.10 | 6.30 | 1.40 |

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kubaini maana na matumizi ya methali za Kiswahili. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili ni cha wastani. **Jedwali 2.11** linaonesha asilimia ya majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo. Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 471,027 sawa na asilimia 51.40 walichagua jibu sahihi *C Vitu vya thamani hupatikana kwa jasho.* Uteuzi wa jibu hilo unaonesha kuwa watahiniwa walikuwa na uelewa wa maana na matumizi ya methali za Kiswahili. Hivyo, maana ya methali hiyo ni ‘mambo mazuri hupatikana kwa kufanya kazi kwa juhudi’.

Jumla ya watahiniwa 433,185 sawa na asilimia 47.2 walichagua vipotoshi *A Ubora wa kitu hautegemei upya wake*, *B Vitu vinavyoelea baharini ni meli, D Vitu vimeumbwa ili vielee* na *E Vitu vya thamani vimeundwa.* Takwimu zinaonesha watahiniwa 287,377 sawa na asilimia 31.30 walichagua kipotoshi A *Ubora wa kitu hautegemei upya wake* kutokana na kushabihisha methali hiyo na ubora wa kitu badala ya kubaini maana ya methali husika. Aidha, kipotoshi hicho kilichaguliwa zaidi na watahiniwa kwa kuwa ndilo chaguo pekee ambalo halikuanza na neno vitu. Uteuzi wa kipotoshi *B, Vitu vinavyoelea baharini ni meli,* watahiniwa walielewa kuwa meli ndio inayoelea baharini. Vilevile, watahiniwa waliochagua kipotoshi *E Vitu vya thamani vimeundwa* walielewa kuwa vitu vizuri huwa

vinatengenezwa. Kwa jumla, watahiniwa waliochagua vipotoshi vyote hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana na matumizi ya methali za Kiswahili katika mazingira ya kila siku.

## 2.3 Sehemu C: Ufahamu

Katika sehemu hii, watahiniwa walitakiwa kusoma kifungu cha habari na kujibu maswali yaliyotokana na habari hiyo. Kifuatacho ni kifungu cha habari walichopewa watahiniwa.

*Jua lilikuwa linaunguza mithili ya moto. Hapakuwa na nyasi wala miti iliyokuwa na majani ya rangi ya kijani. Kila uoto ulikuwa wa rangi ya kahawia kavu! Aidha, kupata tone la maji ya kunywa ilikuwa ndoto kwani mito na visima vyote vilikauka kau. Baada ya kuhangaika kwa njaa na kiu, ndipo wanyama waliamua waitishe mkutano ili wajadili hatua ya kuchukua. Makundi ya wanyama wa aina na ukubwa mbalimbali walikutana chini ya mbuyu. Swala, nyani, mbawala na tembo wote walikuwepo.*

*"Kama mjuavyo mimi ndimi mfalme wa wanyama wote. Ningurumapo hapana achezaye. Kwa hiyo bila shaka mtakubali kuwa mimi ndiye mwenyekiti wa mkutano huu," alitangaza simba. Wanyama wote walitazamana na kutikisa vichwa kwa ishara ya kuafiki. Kisha nyati alisimama na kusema, "Mheshimiwa mwenyekiti, jana nilisikia mrindimo toka upande wa Magharibi. Hivyo ninashauri sote tuhame na kuelekea upande huo ili tuokoe maisha yetu kwani huko kuna dalili ya mvua." Wanyama wote waliunga mkono hoja hiyo, isipokuwa kobe ambaye alisema, "Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo kweli tumeazimia kuhama, sisi akina kobe tunaomba mtubebe kwani kasi yetu ya kutembea ni ndogo mno."*

*Baada ya kila mnyama kutoa rai yake, Mwenyekiti alisimama na kusema, "Nimesikia yote mliyosema. Kabla ya kuanza kuhama nakutuma wewe ng'ombe upeleke ujumbe wetu kwa binadamu ili*

*waache kuharibu mazingira, kwani hicho ndicho kiini cha matatizo yanayotusibu. Wewe ni kiungo baina yetu na binadamu." Ng'ombe alikubali.*

*Baada ya kufikisha ujumbe ule, binadamu alijibu kuwa alikwishaelewa tatizo la mazingira na tayari alikuwa na mpango kabambe wa kuchinja mifugo yote ili kutekeleza ushauri wa wataalamu wa mazingira wa kuiokoa dunia na janga la jangwa. Kusikia hayo, ng'ombe alichanja mbuga kuelekea kwa wanyama wengine.*


**Swali la 31:** Kwa mujibu wa habari uliyosoma, mkutano wa wanyama ulifanyika wapi?

A. kwa mfalme
B. kisimani
C. chini ya mbuyu
D. kwenye majani
E. jangwani

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa wa kuchambua maudhui ya habari aliyoisoma. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili ni kizuri. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri na watahiniwa wengi. Watahiniwa 760,647 (82.90%) walichagua jibu sahihi *C Chini ya mbuyu* ambako ndiko wanyama walikokutana kwa ajili ya kufanya mkutano. Uchaguzi wa jibu sahihi unaonesha kuwa watahiniwa walikuwa na ufahamu wa kutosha wa kuchambua maudhui ya kifungu cha habari walichopewa.

Watahiniwa wengine 145,641 ambao ni sawa na asilimia 15.8 walishindwa kubaini mandhari ya mkutano wa wanyama. Watahiniwa hao walichagua vipotoshi *A Kwa mfalme, B Kisimani, D Kwenye majani* na *E Jangwani*. Miongoni mwao, waliochagua kipotoshi *A, Kwa mfalme* inaashiria walielewa kuwa mfalme ndiye mwenyekiti hivyo

mkutano ulifanyikia kwake. Uteuzi wa vipotoshi *B, Kisimani, D, Kwenye majani na E, Jangwani* unaonesha watahiniwa walihusianisha mandhari hizo na hali ya ukame uliotokea baada ya kukosekana kwa mvua ambapo, visima vilikauka, majani ya miti yalibadilika rangi na dunia ilikuwa jangwa. Uteuzi huo unadhihirisha kuwa watahiniwa hawakuwa na ufahamu wa kuchambua maudhui ipasavyo katika kifungu cha habari. **Kielelezo 2.14** kinaonesha asilimia ya majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.





**Kielelezo 2.14:** *Kinaonesha kiwango kizuri cha kufaulu ambapo asilimia 82.90 ya watahiniwa waliweza kubaini mahali mkutano wa wanyama ulipofanyikia kuwa ni* "chini ya mbuyu"*.*

**Swali la 32:** Mwenyekiti wa mkutano wa wanyama alikuwa nani?

A. Ng'ombe
B. Kobe
C. Nyati
D. Simba
E. Nyani

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kuhusisha maudhui yanayotokana na kifungu cha habari alichokisoma. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa waliojibu swali hili ni kizuri. Watahiniwa wengi (787,651) sawa na asilimia 85.89 walichagua jibu sahihi *D Simba*. Uteuzi huu unatokana na maarifa waliyonayo katika kuhusisha maudhui na kifungu cha habari na kuweza kutambua kuwa Simba ndiye mnyama mkali na mwenye mamlaka yote na hufahamika zaidi kuliko wanyama wengine na hivyo kuwavutia zaidi watahiniwa.

Watahiniwa wachache ambao ni 118,859 sawa na asilimia 12.96 walichagua vipotoshi *A Ng'ombe, B Kobe, C Nyati* na *E Nyani.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi *B Kobe* walihusisha na kitendo cha kubebwa kwa Kobe kutokana na kasi yake ndogo hivyo, wakavutiwa kuwa ndiye mfalme. Uteuzi wa kipotoshi *C, Nyati* uliwavutia watahiniwa kwa kuwa ndiye aliyetoa hoja ya kuhamia upande wa pili na wanyama wote wakaafiki. Aidha, watahiniwa waliochagua vipotoshi *A Ng'ombe* na *E Nyani* hawakuwa na ufahamu kuwa Ng'ombe alionesha uoga wa kuchinjwa na binadamu na Nyani alitajwa kama mwakilishi katika mkutano*.* Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na ujuzi wa kutosha kuchambua maudhui na kuhawilisha maarifa katika kifungu cha habari. **Kielelezo 2.15** kinaonesha asilimia ya kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa waliojibu swali hili.




**Kielelezo 2.15:** *Kinaonesha kiwango kizuri cha kufaulu ambapo asilimia 85.89 ya watahiniwa waliweza kubaini kuwa Simba ndiye mwenyekiti wa kikao.*

**Swali la 33:** Hali ya kukauka kwa mito, visima, nyasi na miti inayotokana na ukosefu wa mvua inaitwaje?

A. ukame
B. uoto
C. kahawia
D. joto
E. janga

**Jedwali 2.12: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 614,118 | 64,530 | 73,106 | 29,147 | 124,549 | 11,636 |
| Asilimia ya watahiniwa | 66.96 | 7.04 | 7.97 | 3.18 | 13.58 | 1.27 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa kuhusu uelewa wa maudhui katika kifungu cha habari. Swali hili lilijibiwa vizuri kama **Jedwali 2.12** linavyoonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa.

Watahiniwa 614,118 (66.96%) waliweza kuchagua jibu sahihi *A Ukame* lenye maana ya hali ya kukauka kwa ardhi kutokana na kukosekana kwa mvua na kukauka kwa mazao. Watahiniwa hao waliweza kuhusisha jibu hilo na maudhui yaliyopo kifungu cha habari.

Hata hivyo, watahiniwa wachache, 291,332 sawa na asilimia 31.77 walichagua vipotoshi *B Uoto,* C *Kahawia, D Joto* na *E Janga.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi *B Uoto* walihusisha na matokeo ya kukosa mvua yaliyosababisha mimea kutoota. Uteuzi wa C *Kahawia* ulionesha kuwa watahiniwa walihusisha na matokeo ya kukosekana kwa mvua na hivyo mimea kubadilika rangi. Kipotoshi *D Joto* kilionesha kuwa watahiniwa walihusisha joto kama athari ya kukosa mvua. Aidha, watahiniwa 124,549 (13.58%) waliochagua kipotoshi *E Janga* walivutiwa na neno 'janga' kwa sababu maelezo ya swali yanashabihisha hali mbaya (janga) iliyotokana na ukosefu wa mvua. Kwa jumla, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na maarifa ya kutosha katika kuchambua maudhui hususan katika kifungu cha habari na kuhusianisha mazingira halisi.

**Swali la 34:** Jina lingine la mnyama aliyewashauri wanyama wote kuhamia upande ambako kulikuwa na dalili ya mvua ni lipi kati ya yafuatayo?


A. Ndovu
B. Ngwena
C. Mbega
D. Kima
E. Mbogo

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua matumizi ya maneno yenye maana sawa (visawe) katika habari aliyosoma. Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa ni cha wastani, kwani

watahiniwa 518,231 sawa na asilimia 56.51 ndio walichagua jibu sahihi *E Mbogo*. Watahiniwa hao waliweza kushabihisha Mbogo na Nyati ambapo:

> Mbogo ni mnyama mkubwa wa porini mithili ya ng'ombe mwenye pembe kubwa zilizokunjika na Nyati ni mnyama mkubwa wa nchi kavu wa jamii ya ng'ombe anayeishi porini mwenye pembe zilizopinda kuelekea juu.

Kwa upande mwingine, jumla ya watahiniwa 384,462 sawa na asilimia 41.92 waliokosa swali hili walichagua vipotoshi *A Ndovu, B Ngwena, C Mbega* na *D Kima*. Kupitia uteuzi wa vipotoshi hivyo, watahiniwa walichagua jibu *A Ndovu* kwa kutokuelewa kuwa ndovu ni kisawe cha Tembo ambaye alishiriki mkutano bila kutoa ushauri wowote. Watahiniwa waliochagua jibu *B Ngwena* hawakujua kuwa Ngwena ni mnyama mkubwa jamii ya mamba na ambaye hakuwa miongoni mwa wanyama waliohudhuria. Uteuzi wa vipotoshi *C Mbega* na *D Kima* ulitokana na kutokuelewa kuwa mbega na kima ni wanyama wadogo walio katika jamii moja na sio wanyama wakubwa kulingana na muktadha wa kifungu cha habari. Hivyo, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivi hawakuwa na maarifa ya kutosha katika kuchambua maudhui katika kifungu cha habari. **Kielelezo 2.16** kinaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Kielelezo 2.16:** *Kinaonesha kiwango kizuri cha kufaulu ambapo asilimia 56.51 ya watahiniwa waliweza kubaini neno 'nyati' lenye maana sawa na mbogo.*

**Swali la 35:** Katika habari uliyosoma sababu iliyomfanya Kobe kutoafiki moja kwa moja hoja ya kuhama ni ipi?

A. Alikuwa mpinzani wa mwenyekiti
B. Aliogopa kuachwa nyuma
C. Kulikuwa na jua kali
D. Wanyama wengine wangeweza kumla
E. Kobe ni mvivu kutembea

**Jedwali 2.13: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 53,744 | 454,888 | 48,728 | 35,437 | 313,925 | 10,364 |
| Asilimia ya watahiniwa | 5.86 | 49.60 | 5.31 | 3.86 | 34.23 | 1.13 |

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kuchambua maudhui ya habari aliyoisoma. **Jedwali 2.13** linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa na kiwango cha kufaulu ambacho kilikuwa cha wastani.

Watahiniwa 454,888 sawa na asilimia 49.60 waliweza kuchagua jibu sahihi *B Aliogopa kuachwa nyuma.* Uteuzi wa jibu hilo unadhihirisha kuwa watahiniwa walikuwa na maarifa ya kutosha katika kuchambua maudhui ya kifungu cha habari.

Hata hivyo, watahiniwa wengine 451,834 (49.27%) walichagua vipotoshi *A Alikuwa mpinzani wa mwenyekiti, C Kulikuwa na jua kali, D Wanyama wengine wangeweza kumla* na *E Kobe ni mvivu kutembea.* Watahiniwa wengi, 313,925 (34.23%) waliochagua kipotoshi *E Kobe ni mvivu kutembea* walivutiwa na ombi la kubebwa kwa kobe kwa kuwa kasi yake ya kutembea ni ndogo. Aidha, watahiniwa waliochagua kipotoshi *A Alikuwa mpinzani wa mwenyekiti* walihusianisha na kitendo cha kobe kutokuafiki kuhama hadi abebwe. *C Kulikuwa na jua kali,* walihusianisha na kutoafiki kwa kobe kutokana kuogopa jua kali na uteuzi *D Wanyama wengine wangeweza kumla* haukuwa na uhusiano wowote na kifungu cha habari. Kwa jumla, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na maarifa ya kutosha katika uchambuzi wa maudhui ya kifungu cha habari.


**Swali la 36:** Kwa mujibu wa habari hii, uharibifu mkubwa wa mazingira hufanywa na nani?

A. Tembo
B. Mbawala
C. Swala
D. Binadamu
E. Nyani

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kuchambua maudhui ya habari aliyoisoma. Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo idadi kubwa ya watahiniwa 787,708 sawa na asilimia

85.89 waliweza kuchagua jibu sahihi *D Binadamu* kutokana na uwezo wa kuchambua maudhui katika kifungu cha habari.

Watahiniwa wengine, 119,206 sawa na asilimia 13 walichagua vipotoshi *A Tembo, B Mbawala, C Swala* na *E Nyani*. Vipotoshi hivyo vinahusisha makundi ya wanyama walioshiriki katika mkutano lakini hawakutuhumiwa kuharibu mazingira. Kwa jumla, majibu hayo yasiyo sahihi yanaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuchambua maudhui katika habari waliyosoma. Mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa umeoneshwa katika **Kielelezo 2.17**.




**Kielelezo 2.17**: *Kinaonesha kiwango kizuri cha kufaulu ambapo asilimia 85.89 ya watahiniwa waliweza kubaini kuwa uharibifu wa mazingira hufanywa na binadamu.*

**Swali la 37:** Neno lipi kati ya yafuatayo lina maana sawa na neno janga?

A. Maafa
B. Kiu
C. Ukame
D. Jangwa
E. Joto

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kuchambua maudhui ya habari ili kutambua maneno yenye maana zinazofanana. Swali hili halikujibiwa vizuri hivyo kufanya kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa kuwa hafifu. Watahiniwa 498,576 sawa na asilimia 54.36 walichagua vipotoshi *B Kiu, C Ukame, D Jangwa* na *E Joto*. Miongoni mwao, watahiniwa 39,393 (4.30%) walichagua kipotoshi *B Kiu* chenye maana ya hisia ya mwili ya kutamani kupata maji bila kutambua kuwa 'janga' ni madhara ya kukosa mvua. Watahiniwa wengine 435,095 (47.4%) walichagua vipotoshi *C Ukame* na *D Jangwa* kutokana na kuvutiwa na maneno hayo yenye maana inayokaribiana na janga ambayo kwa jumla ni matokeo ya kukosa mvua ambapo ni tofauti na janga ambalo ni tukio la hatari linalosababisha maafa. Aidha, watahiniwa 24,088 (2.63%) walichagua kipotoshi *E Joto* chenye maana ya hali ya kuwa na fukuto kutokana na jua kali. Kwa jumla, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na maarifa ya kutosha katika kuchambua maudhui ili kubaini maana sawa za maneno.

Hata hivyo, watahiniwa 406,527 sawa na asilimia 44.33 walichagua jibu sahihi *A Maafa* lenye maana ya madhara makubwa yaliyotokana na ukame. Watahiniwa waliochagua jibu hilo wameonesha kuwa na maarifa ya kutosha katika kuchambua maudhui katika habari waliyosoma na kuweza kutambua kuwa neno 'janga' lina maana sawa na maafa. Aidha, watahiniwa 11,983 (1.31%) walichagua jibu zaidi ya moja na wengine hawakuchagua jibu lolote.


**Swali la 38:** Kifungu cha maneno "alichanja mbuga" kina maana gani?

A. alijirudi
B. alitembea
C. alikimbia
D. alirudi

E. aliruka

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kuchambua maudhui ili kupata maana ya msemo kama ulivyotumika katika kifungu cha habari. Kiwango cha kufaulu kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 631,245 sawa na asilimia 68.83 waliweza kuchagua jibu sahihi *C Alikimbia*. Uteuzi huo unathibitisha kuwa watahiniwa walikuwa na maarifa ya kutosha katika kuchambua maudhui na kupata maana ya msemo 'alichanja mbuga' wenye maana ya kuondoka mahali kwa kasi.

Hata hivyo, watahiniwa 274,284 sawa na asilimia 29.91 walichagua vipotoshi *A alijirudi, B alitembea, D alirudi* na *E aliruka.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi *A alijirudi*, hawakuelewa kuwa neno hilo lina maana ya kumsihi mtu ajirekebishe kwa jambo baya alilofanya, jambo ambalo halikujitokeza katika habari waliyoisoma. Aidha, watahiniwa walioteua kipotoshi *B alitembea* ambacho hakiakisi maana halisi ya kuondoka kwa kasi bali kinamaanisha kutembea kwa kawaida. Baadhi ya watahiniwa waliochagua kipotoshi *D alirudi* hawakuelewa kuwa, kipotoshi hicho hakihusiani na hali ya kwenda kwa kasi. Aidha, watahiniwa wachache walichagua kipotoshi *E aliruka* kwa kushindwa kubaini kuwa neno hilo lina maana ya kutoka chini kwenda hewani ambako hakuhusiani na hali ya kwenda kwa kasi au kukimbia. Kwa jumla, uteuzi wa vipotoshi hivyo, vyenye tofauti na kifungu cha maneno 'alichanja mbuga' haukuwa sahihi. Hivyo, watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha katika uchambuzi wa maudhui katika kifungu cha habari. **Kielelezo 2.18** kinaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Kielelezo 2.18**: *Kinaonesha kiwango kizuri cha kufaulu ambapo asilimia 68.83 ya watahiniwa waliweza kubaini maana ya kifungu cha maneno alichanja mbuga chenye maana ya kukimbia.*


**Swali la 39:** Binadamu alikusudia kuchinja wanyama wa aina gani?

A. Wanyama pori wote
B. Ng'ombe na simba
C. Wanyama wadogo wote
D. Wanyama wakubwa wote
E. Wanyama wote wanaofugwa

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kuchambua maudhui ya habari aliyoisoma. Swali hili lilijibiwa vizuri na watahiniwa 581,257 sawa na asilimia 63.38 kwa kuchagua jibu sahihi *E Wanyama wote wanaofugwa.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha katika kuchambua maudhui katika kifungu cha habari. Kundi la wanyama wanaofugwa linahusisha, ng'ombe, mbuzi na kondoo.

Hata hivyo, watahiniwa 323,420 sawa na asilimia 35.27 walichagua vipotoshi *A wanyama pori wote, B Ng'ombe na Simba, C Wanyama wadogo wote* na *D Wanyama wakubwa wote.* Uteuzi wa vipotoshi

hivyo unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu uchambuzi wa maudhui na jinsi unavyoshabihiana na mazingira halisi. Watahiniwa wengi, 195,598 (21.33%) walichagua kipotoshi *A wanyama pori wote,* kuwa ndio watakaochinjwa na binadamu, hali inayoonesha hawakuelewa wanyama wa kufugwa ni wepi. Watahiniwa, waliochagua vipotoshi *B Ng'ombe na Simba, C Wanyama wadogo wote* na *D Wanyama wakubwa wote* hawakuwa na maarifa ya kutosha katika kusoma kifungu cha habari kwa ufahamu. **Kielelezo 2.19** kinaonesha kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika kila chaguo.




**Kielelezo 2.19**: *Kinaonesha kiwango kizuri cha kufaulu ambapo asilimia 63.38 ya watahiniwa waliweza kubaini jibu sahihi kuwa binadamu anakukusudia kuchinja Wanyama wote wanaofugwa*

**Swali la 40:** Kichwa cha habari uliyosoma kingefaa kiwe kipi?

A. Kiangazi na jangwa
B. Matatizo ya binadamu
C. Jua kali
D. Uhamisho wa wanyama
E. Uharibifu wa mazingira

**Jedwali 2.14: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 93,100 | 49,089 | 142,917 | 67,506 | 552,123 | 12,351 |
| Asilimia ya watahiniwa | 10.15 | 5.35 | 15.58 | 7.36 | 60.20 | 1.35 |

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kuchambua maudhui ili kubaini kichwa cha habari. **Jedwali 2.14** linaonesha majibu ya watahiniwa katika swali hili. Takwimu zinaonesha kuwa kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 552,123 sawa na asilimia 60.20 waliweza kuchagua jibu sahihi *E Uharibifu wa mazingira*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuchambua maudhui na kubaini kichwa cha habari kutokana na kuelewa sababu ya wanyama kuitisha mkutano.

Hata hivyo, jumla ya watahiniwa 352,612 sawa na asilimia 38.6 ya watahiniwa walichagua vipotoshi *A kiangazi na jangwa, B Matatizo ya binadamu, C Jua kali* na *D uhamisho wa wanyama.* Watahiniwa hao walishindwa kuoanisha maudhui na kichwa cha habari. Aidha watahiniwa 96,959 (10.57%) waliochagua vipotoshi *A kiangazi na jangwa* na *C Jua kali* walielewa kuwa “kiangazi na jangwa” na “jua kali” ni madhara yaliyotokana na ukosefu wa mvua hivyo kuvutiwa kuchagua vipotoshi hivyo kuwa kichwa cha habari. Uteuzi wa vipotoshi *B Matatizo ya binadamu* na *D Uhamisho wa wanyama,* unaashiria kuwa watahiniwa walielewa kuwa binadamu ni chanzo cha matatizo yaliyowakabili wanyama kunakohusiana na kuhama kwa wanyama hao. Kwa jumla, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu uchambuzi wa maudhui unaosaidia kupata kichwa cha habari.

## 2.4 Sehemu D: Ushairi

Katika sehemu hii watahiniwa walitakiwa kusoma shairi lifuatalo na kujibu maswali yanayotokana na shairi hilo.

Kuku kapewa uwezo, kutaga na kuangua,
Yai uache mizozo, kuchunguza asilia,
Ungegeuka uozo, kuku angekuziria,
Yai wewe ni mtoto, kuku kwako ndiye mama.


**Swali la 41**: Kituo cha shairi hili ni kipi?

A. Kuku kapewa uwezo, kutaga na kuangua
B. Yai wewe ni mtoto
C. Ungegeuka uozo, kuku angekuziria
D. Kuku kwako ndiye mama
E. Yai wewe ni mtoto, kuku kwako ndiye mama

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu muundo wa shairi katika lugha ya Kiswahili. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 655,155 sawa na asilimia 71.44 walichagua jibu sahihi *E Yai wewe ni mtoto, kuku kwako ndiye mama.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kituo cha shairi kuwa ni mstari wa mwisho wa ubeti katika shairi.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha pia kuwa jumla ya watahiniwa 249,336 sawa na asilimia 27.19 walichagua kati ya vipotoshi *A Kuku kapewa uwezo, kutaga na kuangua, B Yai wewe ni mtoto, C Ungegeuka uozo, kuku angekuziria* na *D Kuku kwako ndiye mama*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *A Kuku kapewa uwezo, kutaga na kuangua,* hawakuwa na maarifa ya kutosha katika kubaini kituo cha shairi. Aidha, wao waliona kuwa mstari huo ndio kituo cha shairi kwa kuwa ni wa kwanza katika ubeti huo kinyume na uhalisia kuwa kituo ni mstari wa mwisho wa ubeti wa shairi. Uteuzi wa

kipotoshi *B Yai wewe ni mtoto* inaonesha watahiniwa walielewa kuwa kituo ni mstari wa mwisho katika kipande cha kwanza cha ubeti, na waliochagua kipotoshi *D Kuku kwako ndiye mama* walielewa kuwa 'kituo' ni mstari wa mwisho wa beti katika kipande cha pili. Hivyo, uteuzi wa vipotoshi vyote unadhihirisha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu uchambuzi wa muundo wa shairi katika kubaini kituo cha shairi. **Kielelezo 2.20** kinaonesha kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili.




**Kielelezo 2.20**: *Kinaonesha kiwango kizuri cha kufaulu ambapo asilimia 71.44 ya watahiniwa waliweza kubaini kituo cha shairi kuwa ni 'yai* wewe ni mtoto, kuku kwako ndiye mama'.


**Swali la 42**: Katika shairi hili vina vya kati na mwisho ni vipi?

A. Zo na ku
B. zo na a
C. to na ku
D. u na ku
E. yu na ku

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu kanuni za utunzi wa mashairi. Takwimu zinaonesha kuwa kiwango cha kufaulu kwa

watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 737,036 sawa na asilimia 80.37 waliweza kuchagua jibu sahihi *B 'zo na a'.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya vina kuwa ni *silabi zinazofanana katikati na mwishoni mwa kila mstari wa ushairi.*

Hata hivyo, watahiniwa 168,772 sawa na asilimia 18.3 walichagua vipotoshi *A zo na ku, C to na ku, D u na ku* na *E yu na ku*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *A 'zo na ku'* walielewa kuwa ni silabi za mwisho katika mistari mitatu ya kwanza kati 'zo' na silabi za mwanzo 'ku' katika kipande cha pili kwa mistari mitatu ya kwanza. Uteuzi wa kipotoshi *C 'to na ku'* na *D 'u na ku'* unaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na ufahamu kuhusu vina katika ubeti wa shairi. Aidha, watahiniwa wachache kati ya hao, walichagua kipotoshi *E yu na ku* ambavyo havikuwepo katika mstari wowote wa ubeti huo. **Kielelezo 2.21** kinaonesha kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili.





**Kielelezo 2.21:** *Kinaonesha kiwango kizuri cha kufaulu ambapo asilimia 80.37 ya watahiniwa waliweza kubaini vina vya kati 'zo' na vya mwisho 'a'.*

**Swali la 43**: Shairi hili lina mizani ngapi?

A. Kumi na sita
B. Minne
C. Nane
D. Ishirini na tatu
E. Sita

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu muundo wa shairi katika lugha ya Kiswahili. Kiwango cha kufaulu katika swali hili ni kizuri, kwani jumla ya watahiniwa 631,550 sawa na asilimia 68.89 waliweza kuchagua jibu sahihi *A kumi na sita*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mizani kuwa ni *jumla ya silabi katika mshororo (mstari) wa shairi.*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 272,475 ( 29.7%) walichagua vipotoshi *B Minne, C Nane, D Ishirini na tatu* na *E Sita* kwa kuwa hawakuwa na maarifa kuhusu mizani katika mashairi. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *B minne*, hawakuwa na maarifa kuhusu mizani bali walibainisha idadi ya mistari katika ubeti, badala ya kutaja idadi ya mizani kwa kila mstari. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *C nane,* walihesabu idadi ya silabi katika kipande kimoja cha mstari na waliochagua kipotoshi *E sita*, walihesabu idadi ya maneno katika mstari wa kwanza wa ubeti husika na kupata idadi ya maneno sita badala ya kuhesabu mizani. Uteuzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu muundo wa shairi hususan katika dhana ya mizani. **Kielelezo 2.22** kinaonesha kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili.




**Kielelezi 2.22:** *Kinaonesha kiwango kizuri cha kufaulu ambapo asilimia 68.86 ya watahiniwa waliweza kubaini mizani kumi na sita ndani ya shairi.*

**Swali la 44**: Shairi hili lina beti ngapi?

A. Nne
B. Nane
C. Moja
D. Mbili
E. Kumi na sita

**Jedwali 2.15: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 102,821 | 37,492 | 708,853 | 32,925 | 24,112 | 10,883 |
| Asilimia ya watahiniwa | 11.21 | 4.09 | 77.29 | 3.59 | 2.63 | 1.19 |

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu muundo wa shairi katika lugha ya Kiswahili. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri. Mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa umeoneshwa katika **Jedwali Na. 2.15**. Watahiniwa 708,853 sawa na asilimia 77.29 walichagua jibu sahihi *C Moja*. Uchambuzi uliofanyika

unaonesha kuwa watahiniwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu muundo wa ubeti wa shairi. Ubeti katika shairi ni kifungu cha maneno kilichopangwa kwa mishororo miwili au zaidi. Kupitia shairi lililotolewa kwa watahiniwa, kulikuwa na kifungu kimoja tu chenye mishororo minne, hivyo watahiniwa waliweza kubaini ubeti wa shairi kwa usahihi.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa 197,350 sawa na asilimia 21.52 walichagua vipotoshi *A Nne, B Nane, D Mbili na E Kumi na sita.* Uteuzi wa vipotoshi hivyo unadhihirisha kuwa watahiniwa hawakuwa na uelewa wa beti katika muundo wa shairi. Aidha, watahiniwa wachache waliochagua kipotoshi *A Nne* walihesabu mishororo katika ubeti badala ya kutaja idadi ya beti. Kipotoshi *B Nane* kinaonesha watahiniwa walitumia kigezo cha idadi ya maneno katika mstari wa mwisho ambayo ni nane. Mwisho, watahiniwa waliochagua vipotoshi *D Mbili* na *E Kumi* wanadhihirisha hawakuelewa kuhusu beti katika mashairi kwani hakuna uhusiano wowote na idadi ya beti katika shairi walilopewa. Kwa jumla, uteuzi wa vipotoshi vyote unaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na uelewa kuhusu beti katika mashairi.

**Swali la 45**: Neno “kuangua” kama lilivyotumika katika shairi hili lina maana ipi?

A. Kuvunja mayai
B. Kula mayai
C. Kukwangua mayai
D. Kutoa vifaranga katika mayai
E. Kulalia mayai


Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu maana na matumizi ya msamiati katika shairi. Takwimu zinaonesha kuwa kiwango cha

kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 656,441 sawa na asilimia 71.58 waliweza kuchagua jibu sahihi *D kutoa vifaranga katika mayai.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya neno 'kuangua' na jinsi lilivyotumika katika shairi. Kuangua ni kitendo cha kufanya kinda au kifaranga kitoke chenyewe katika yai la ndege kama kuku, bata au kasuku. Hivyo maarifa waliyokuwa nayo watahiniwa yaliwawezesha kubaini kwa usahihi maana ya neno kuangua.

Kwa upande mwingine, jumla ya watahiniwa 248,458 sawa na asilimia 27.09 walichagua vipotoshi *A kuvunja mayai, B kula mayai, C kukwangua mayai* na *E kulalia mayai.* Aidha, watahiniwa waliochagua *vipotoshi hivyo* hawakuelewa maana ya vitenzi vilivyobeba nomino mayai. Vitenzi hivyo ni :

> 'vunja' ikiwa na maana ya pasua vipande vipande au sambaratisha, 'kula' ni kuingiza kitu kinywani, 'kukwangua' ni kuondoa kitu kwa kukwaruza na 'kulalia' ni kuatamia mayai kwa ndege na baadhi ya wanyama wanaotambaa.

Uteuzi wa vipotoshi hivyo umebaini kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana na matumizi ya msamiati katika shairi ukilinganisha na mazingira halisi. Mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa umeoneshwa katika **Kielelezo 2.23**.




**Kielelezo Na. 2.23**: *Kinaonesha kiwango kizuri cha kufaulu ambapo asilimia 71.58 ya watahiniwa waliweza kubaini maana ya kuangua kuwa ni kutoa kifaranga kwenye mayai.*

**Swali la 46**: Neno "mizozo" kama lilivyotumika katika shairi hili lina maana gani?

A. Ghasia
B. Udadisi
C. Woga
D. Majigambo
E. Utafiti

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu maana na matumizi ya msamiati katika shairi. Takwimu zinaonesha kuwa swali hili ni miongoni mwa maswali ambayo hayakujibiwa vizuri. Watahiniwa 564,155 sawa na asilimia 61.52 walichagua vipotoshi *B Udadisi, C Woga, D Majigambo* na *E Utafiti.* Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana na matumizi ya msamiati katika shairi walilopewa. Aidha, watahiniwa 165,536 (18.05%) waliochagua kipotoshi *B Udadisi* na watahiniwa 69,245 (7.55%) kipotoshi *E Utafiti*, walikosa maarifa kuhusu maana za maneno hayo kwani 'udadisi' na

'utafiti' yana maana ya kufanya uchunguzi wa jambo lisilojulikana kwa lengo la kubaini ukweli au kupata maarifa mapya. Vivyo hivyo, watahiniwa 246,010 (26.83%) walichagua kipotoshi *D Majigambo* lenye maana ya hali ya kutoa maneno ya kujisifia au kujikweza. Aidha, watahiniwa wachache 83,364 (9.09%) walichagua kipotoshi *C Woga,* neno lenye maana ya hisia ya kujawa na hofu ya kupatwa na jambo baya. Kwa jumla, vipotoshi hivyo vina maana isiyowiana na jibu sahihi 'ghasia' ambayo ni tukio la fujo na vurugu.

Hivyo basi, watahiniwa wachache 338,220 sawa na asilimia 36.88 ndio walioweza kuchagua jibu sahihi *A Ghasia.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya msamiati huo kuwa ni tukio la vurugu na fujo linalosababisha kutokuwepo kwa hali ya amani. Maana hii inahusiana na ile ya mizozo ambayo ni kutokubaliana katika jambo baina ya watu kunakosababisha kutupiana maneno, kelele nyingi na vurugu. Aidha, watahiniwa 14,711 (1.60%) walichagua jibu zaidi ya moja na wengine hawakuchagua jibu lolote.

## 2.5 Sehemu E: Utungaji

Katika sehemu hii, watahiniwa walipewa sentensi nne (4) zilizoandikwa bila mtiririko sahihi na walitakiwa wazipange sentensi hizo ili ziwe na mtiririko wenye mantiki kwa kuzipa herufi A, B, C na D.

**Jedwali Na. 2.16**: **Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo**

| Swali | Jibu Sahihi | Idadi ya Watahiniwa | Asimilia ya Watahiniwa | Mengine (%) | Jibu E (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| **48** | A | 659,860 | 72.0 | 1.1 | 1.4 |
| **49** | B | 624,037 | 68.0 | 1.1 | 1.5 |
| **47** | C | 653,967 | 71.3 | 1.2 | 1.5 |
| **50** | D | 666,397 | 72.7 | 1.1 | 3.1 |

**Swali la 47:** Zizi hilo limegawanywa katika sehemu mbili.

**Swali la 48:** Baba yangu anafuga ng'ombe, mbuzi na kondoo.

**Swali la 49:** Nje ya nyumba yetu kuna zizi kubwa.

**Swali la 50:** Sehemu moja ni ya ng'ombe na nyingine ni ya mbuzi na kondoo.

Sehemu hii ililenga kupima uwezo wa watahiniwa katika upangaji wa mawazo katika mtiririko wenye mantiki. **Jedwali 2.16** linaonesha kuwa kiwango cha kufaulu cha watahiniwa kilikuwa kizuri kwani idadi kubwa ya watahiniwa walimudu kupanga kwa usahihi sentensi ya kwanza hadi ya mwisho. Watahiniwa 659,860 (71.95%) waliweza kupanga sentensi ya kwanza (Na. 48) kwa usahihi kwa kuandika herufi 'A'. Vivyo hivyo, watahiniwa 624,037 sawa na asilimia 68.05 walipanga na kuandika sentensi ya pili (Na.49) kwa usahihi wa herufi 'B'. Hali kadhalika, watahiniwa 653,967 sawa na asilimia 71.31 waliweza kupanga sentensi ya tatu (Na. 47) kwa kuandika herufi 'C' na katika kukamilisha sentensi ya mwisho, watahiniwa 666,397 sawa na asilimia 72.66 walipanga sentensi ya nne (Na. 50) na kuandika herufi 'D' kwa usahihi. Kiwango hiki cha kufaulu kwa watahiniwa katika kupanga sentensi hizo kinadhihirisha wazi kuwa watahiniwa walikuwa

na maarifa na uelewa wa kutosha kuhusu utungaji wa habari fupi zenye mantiki.

Licha ya sehemu hii kujibiwa vizuri na idadi kubwa ya watahiniwa, wapo wachache (68,985) sawa na asilimia 7.53 waliojibu maswali haya kama yale ya kuchagua kwa kujaza vipengele A hadi D, na E ambacho hakikuwepo kwenye maelekezo bila kufuata mtiririko sahihi. Watahiniwa hao hawakuelewa maelekezo ya swali pia inaelekea kuwa walikosa maarifa ya kupanga herufi kuanzia A hadi D kwa mtiririko jambo lililosababisha kuandika herufi E ambayo si miongoni mwa herufi walizopaswa kuziandika katika kupanga sentensi hizo nne.

## 3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA MADA MBALIMBALI

Mada zilizotahiniwa katika somo la Kiswahili ni *Sarufi*, *Lugha ya Kifasihi*, *Ufahamu*, *Ushairi* na *Utungaji*. Uchambuzi wa kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa kwa kila mada kinaonesha kuwa, mada zote zilikuwa na kiwango kizuri cha kufaulu. Mada iliyokuwa na kiwango cha juu zaidi ilikuwa ni mada ya *Utungaji* (71.00%) ikifuatiwa na mada ya *Ushairi* (67.75%), *Ufahamu* (66.45), *Sarufi* (61.17%) na *Lugha ya Kifasihi* (60.40%). Uchambuzi unaonesha kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri na watahiniwa katika mada ya *Sarufi* ni maswali manne; Swali la 1 (90.44%), 19 (88.73%), 17 (81.70%) na la 10 (80.15). Katika mada ya *Lugha ya Kifasihi*, swali la 28 (89.72%), la 27 (80.85%) na la 21 (70.38%). Aidha, katika mada ya *Ufahamu*, swali la 32 (85.89%) na 31 (82.90%) yalikuwa na kiwango kizuri cha kufaulu. Pia, katika mada ya *Ushairi* maswali yaliyojibiwa vizuri ni swali la 42 (80.37%) na 44 (77.29%). Mwisho, katika mada ya

*Utungaji*, swali la 50 (72.66%) lilijibiwa vizuri. Kwa jumla, swali lililojibiwa vizuri zaidi kuliko mengine katika mada zote ni swali la 1 (90.44%) kutoka katika mada ya *Sarufi*.

Licha ya viwango vizuri vya kufaulu kwa maswali mengi, yapo machache yaliyokuwa na viwango hafifu vya kufaulu hususan katika mada ya *Sarufi* ambapo swali la 8 lilikuwa na asilimia 23.56 na la 20 lilikuwa na asilimia 25.38. Aidha, katika mada ya *Ushairi*, swali la 46 lilikuwa na kiwango hafifu cha kufaulu (36.88%). Katika mada ya *Lugha ya Kifasihi*, kiwango hafifu cha kufaulu kilikuwa katika swali la 24 ambapo ni asilimia 14.39 tu ndio walioweza kujibu swali hilo. Hata hivyo, swali hilo lilikuwa na kiwango cha chini zaidi cha kufaulu kuliko maswali mengine katika mada zote. Pia, kutokana na uchambuzi uliofanyika, imebainika kuwa hakuna swali lililokuwa na kiwango hafifu cha kufaulu katika mada ya *Utungaji*.

Ulinganifu wa kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa kwa mada kati ya PSLE 2016 na 2017 kinaonesha kuwepo kwa ongezeko kubwa la kufaulu. Uchambuzi unaonesha kuwa katika mada ya *Sarufi*, wastani wa kufaulu umeongezeka kutoka 57.10 hadi 61.17 kukiwa na ongezeko la asilimia 4.07. Wastani wa kufaulu katika mada ya *Lugha ya Kifasihi* kwa mwaka 2016 ulikuwa hafifu kwa asilimia 39.95, tofauti na mwaka 2017 ambapo wastani wa kufaulu ni 60.40% ukiwa na ongezeko la kufaulu kwa asilimia 20.45. Aidha, katika mada ya *Ufahamu* kiwango cha kufaulu kimeongezeka kutoka asilimia 57.87 kwa mwaka 2016, hadi kufikia asilimia 66.45 kwa mwaka 2017. Hili ni ongezeko la asilimia 8.58 kutoka kiwango cha *wastani* cha kufaulu na kuwa *kizuri.* Katika mada ya *Ushairi,* kiwango cha kufaulu kimeendelea kuwa kizuri. Wastani wa kufaulu kwa watahiniwa kwa

mwaka 2016 ulikuwa asilimia 65.71 na kwa mwaka 2017 ni asilimia 67.75 ambapo kumekuwa na ongezeko la asilimia 2.04. Pia katika mada ya *Utungaji,* wastani wa kufaulu kwa watahiniwa umepanda kutoka kiwango cha *wastani* (47.95%) kwa mwaka 2016, na kuwa kizuri (71.00%) kwa ongezeko la asilimia 23.05.

Uchambuzi wa mada unaonesha kuwepo kwa ongezeko la kufaulu kwa watahiniwa katika mada zote kwa mwaka 2017 ambapo kiwango cha kufaulu kilikuwa kizuri. Hata hivyo, juhudi zaidi zinahitajika ili kuinua kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada mbalimbali. Mada zinazohitaji kutiliwa mkazo zaidi ni mada ndogo ya *Aina za Maneno* (Sarufi) na Methali (*Lugha ya Kifasihi*) kwani maswali yaliyohusiana na mada hizo yalijibiwa kwa kiwango cha chini (hafifu). Uchambuzi wa viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa kila mada katika somo la Kiswahili umewasilishwa katika **kiambatisho A na kiambatisho cha pekee**.

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa viwango vya jinsi watahiniwa walivyojibu maswali umebainisha dosari zilizowafanya watahiniwa washindwe kujibu maswali kwa usahihi. Miongoni mwa dosari hizo ni kushindwa kutambua matakwa ya swali, kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada mbalimbali katika somo, kutokufahamu kanuni za lugha na matumizi ya misamiati, kutokujibu kabisa baadhi ya maswali au kuchagua jibu zaidi ya moja kinyume na maelekezo katika mtihani na kushindwa kuhaulisha mazingira wanamoishi.

Uchambuzi wa mada unaonesha kuwa kiwango cha kufaulu kwa mada zote katika mwaka 2017 kimekuwa kizuri ukilinganisha na

mwaka 2016. Kwa mfano kumekuwa na ongezeko la asilimia 20.45 katika mada ya *Lugha ya Kifasihi* ukilinganisha na wastani wa kufaulu kwa mwaka 2016 ambao ulikuwa hafifu kwa asilimia 39.95 na kuwa kiwango kizuri kwa mtihani wa mwaka 2017 kwa asilimia 60.4. Kwa jumla kiwango cha kufaulu kwa mwaka 2017 ni kizuri kwa wastani wa asilimia 65.35 ambapo asilimia 11.63 imeongezeka ikilinganishwa na wastani wa mwaka 2016 ambapo ulikuwa asilimia 53.72. Pamoja na kuongezeka kwa kiwango cha kufaulu katika mada zote, juhudi za dhati na maarifa zaidi zinahitajika katika ufundishaji na ujifunzaji ili kuinua kiwango cha kufaulu zaidi kwa watahiniwa.

Kiswahili ni lugha ya Taifa na ni sehemu ya utamaduni wa Mtanzania. Lugha ya Kiswahil inaunganisha nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na hutumika kimataifa. Hivyo, kunahitajika juhudi za dhati ili kuimarisha lugha hii kuanzia elimu msingi hadi elimu ya juu. Kwa matokeo ya hayo yote, lugha hii itakuwa imepewa heshima inayostahili kama lugha ya taifa.

## 5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Mambo muhimu yafuatayo yatasaidia kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa kuwajengea watahiniwa ujuzi na maarifa ili kupata matokeo mazuri ya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi.

(a) Walimu wanaofundisha somo la Kiswahili katika shule za msingi wanatakiwa kuzingatia muhtasari katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

(b) Walimu wanatakiwa kutoa mazoezi ya kutosha mara kwa mara katika mada zote, kusahihisha na kutoa mrejesho.

(c) Walimu wawajengee wanafunzi tabia ya kusoma vitabu mbalimbali vya hadithi na kuchambua maudhui ili kupata maarifa mbalimbali hususan katika mada ya ufahamu.

(d) Walimu wawaelekeze wanafunzi jinsi ya kuchagua na kujibu maswali ili kuepuka dosari kwa baadhi ya watahiniwa kutokufanya baadhi ya maswali au kushindwa kuzingatia maelekezo ya maswali.

(e) Walimu wawahamasishe wanafunzi kutumia Kiswahili sanifu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji ili kuboresha msamiati na sarufi ya lugha.

**KIAMBATISHO A**

## ULINGANIFU WA KIWANGO CHA KUFAULU KWA WATAHINIWA KWA KILA MADA KATIKA PSLE 2016 NA PSLE 2017

**01 Kiswahili**

| Na | Mada | PSLE 2016 | | | | PSLE 2017 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Kufaulu (%) | Maoni | Kufaulu kwa kila swali | | Wastani wa Kufaulu | Maoni |
| | | Namba ya Swali | % ya Kufaulu | | | Namba ya swali | % ya Kufaulu | | |
| 1. | Sarufi | 1 | 41.03 | 57.10 | Wastani | 1 | 90.44 | 61.17 | Vizuri |
| | | 2 | 36.26 | | | 2 | 52.58 | | |
| | | 3 | 77.09 | | | 3 | 36.43 | | |
| | | 4 | 42.52 | | | 4 | 48.01 | | |
| | | 5 | 39.16 | | | 5 | 73.38 | | |
| | | 6 | 82.64 | | | 6 | 77.89 | | |
| | | 7 | 31.4 | | | 7 | 30.29 | | |
| | | 8 | 42.83 | | | 8 | 23.56 | | |
| | | 9 | 65.34 | | | 9 | 78.38 | | |
| | | 10 | 87.91 | | | 10 | 80.15 | | |
| | | 11 | 74.17 | | | 11 | 73.26 | | |
| | | 12 | 74.17 | | | 12 | 66.81 | | |
| | | 13 | 52.98 | | | 13 | 70.02 | | |
| | | 14 | 40.56 | | | 14 | 52.01 | | |
| | | 15 | 59.11 | | | 15 | 66.90 | | |
| | | 16 | 79.02 | | | 16 | 62.92 | | |
| | | 17 | 56.27 | | | 17 | 81.70 | | |
| | | 18 | 30.93 | | | 18 | 44.59 | | |
| | | 19 | 65.73 | | | 19 | 88.73 | | |
| | | 20 | 62.79 | | | 20 | 25.38 | | |
| 2. | Lugha ya Kifasihi | 21 | 37.73 | 39.95 | Hafifu | 21 | 70.38 | 60.40 | Vizuri |
| | | 22 | 29.85 | | | 22 | 57.10 | | |
| | | 23 | 25.49 | | | 23 | 52.65 | | |
| | | 24 | 15.71 | | | 24 | 14.39 | | |
| | | 25 | 46.42 | | | 25 | 69.18 | | |
| | | 26 | 54.01 | | | 26 | 49.28 | | |
| | | 27 | 64.81 | | | 27 | 80.85 | | |
| | | 28 | 34.2 | | | 28 | 89.72 | | |
| | | 29 | 39.22 | | | 29 | 68.90 | | |
| | | 30 | 52.03 | | | 30 | 51.40 | | |
| 3. | Ufahamu | 31 | 50.55 | 57.87 | Wastani | 31 | 82.90 | 66.45 | Vizuri |
| | | 32 | 32.79 | | | 32 | 85.89 | | |

| Na | Mada | PSLE 2016 | | | | PSLE 2017 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Kufaulu (%) | Maoni | Kufaulu kwa kila swali | | Wastani wa Kufaulu | Maoni |
| | | Namba ya Swali | % ya Kufaulu | | | Namba ya swali | % ya Kufaulu | | |
| | | 33 | 47.2 | | | 33 | 66.96 | | |
| | | 34 | 76.37 | | | 34 | 56.51 | | |
| | | 35 | 73.16 | | | 35 | 49.60 | | |
| | | 36 | 69.97 | | | 36 | 85.89 | | |
| | | 37 | 76.18 | | | 37 | 44.33 | | |
| | | 38 | 70.87 | | | 38 | 68.83 | | |
| | | 39 | 43.79 | | | 39 | 63.38 | | |
| | | 40 | 37.79 | | | 40 | 60.20 | | |
| 4. | Ushairi | 41 | 70.34 | 65.71 | Mzuri | 41 | 71.44 | 67.75 | Vizuri |
| | | 42 | 79.02 | | | 42 | 80.37 | | |
| | | 43 | 78.69 | | | 43 | 68.86 | | |
| | | 44 | 44.98 | | | 44 | 77.29 | | |
| | | 45 | 45.71 | | | 45 | 71.58 | | |
| | | 46 | 75.51 | | | 46 | 36.88 | | |
| 5. | Utungaji | 47 | 43.9 | 47.95 | Wastani | 47 | 71.31 | 71.00 | Vizuri |
| | | 48 | 36.49 | | | 48 | 71.95 | | |
| | | 49 | 64.36 | | | 49 | 68.05 | | |
| | | 50 | 47.05 | | | 50 | 72.66 | | |

## KIAMBATISHO CHA PEKEE

